SUPA JACKPOT
TZS. 1,104,580,144
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



MAKALA MAALUM:
**Mchechu** na njozi za mageuzi taasisi, mashirika ya umma
UK. 4


MAISHA
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili
MAISHA NI NYUMBA
Eid Pili na wali wa mandi
Using'ang'anie muonekano wa zamani wa nyumba yako
KATUNIKA
'MASCARA' KUNOGESHA MACHO

UKURASA 9

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumapili Aprili 23, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
JUMAPILI
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0581289
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Maadili yatikisa sherehe za Eid

**Rais** aonya kuiga utamaduni wa nje, wazazi wakumbushwa wajibu... *Uk 2 &3*

UKURASA WA 5

## WAZIRI ATANGAZA KUIFUTA KAMPUNI YA MBUNGE UWAKALA WA PEMBEJEO

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe ametangaza kufuta kampuni zaidi ya 700 za mawakala wanaosambaza pembejeo za kilimo kwa wakulima ikiwamo Kinanasi Agri Ltd inayodaiwa kumilikiwa na Mbunge wa Kyela...

## Wastaafu polisi walia mapunjo ya mafao, jeshi lasema ni kweli

UKURASA 5



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na Mufti na Shekhe Mkuu wa Tanzania, Dk. Abubakar Zubeir (wa tatu kulia), Kaimu Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Walid Omar, na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa Kiislamu Tanzania, Shamim Khan, baada ya kuwasili katika Baraza la Eid El-Fitr, Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Samia: Tumepitia wakati mgumu kufikia umoja na mshikamano

UK. 2

MICHEZO SIMBA YATANGULIZA MGUU NUSU FAINALI UK. 24
MAONI, KATUNI UK.6

## Samia: Tumepitia wakati mgumu kufika hapa

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema nchi imepita katika kipindi kigumu hadi kufikia hatua ya sasa ya kuwa na amani, umoja na mshikamano kwa Watanznia kuwa wamoja bila kujali itikadi wala imani zao.

Amesema kipindi cha mwaka jana na mwaka juzi, haikuwa rahisi kwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, kukaa pamoja na viongozi wengine kwenye hafla yoyote lakini sasa wako naye kwa moyo safi.

Rais Samia aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa Baraza la Eid El-Fitr kitaifa lililoandaliwa na Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA) na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali, wakiwamo wanasiasa na viongozi wa dini wa madhehebu tofauti.

"(Mbowe) kapanda juu ya jukwaa kasalimia kwa moyo safi. Huko ndiko tunakotaka kwenda kupitia mafunzo tunayoyapata ndani ya dini zetu," alisema.

Pia alisema amesikia faraja kusikia BAKWATA imeanza kujitathmini kwa sababu taasisi yoyote lazima kuwapo na kujichunguza ili kujitambua imefikia wapi. "Nitoe wito kama ninavyohimiza taasisi za dini, za kiserikali na hata mashirika yasiyo ya kiserikali kuwa na utamaduni huu wa kuongeza tija, yatakayoibuliwa na kamati kama yatahitaji mikono yetu basi tuko tayari kusaidia," aliahidi.

Rais Samia aliwataka kuendeleza ushirikiano na maelewano na makundi mbalimbali ya Waislamu na dini zingine ili kujenga ushirikiano madhubuti na kuheshimiana.

Kuhusu kurasimisha somo la dini shuleni, alisema suala hilo linahusu Katiba na kunukuu Ibara ya 19 (2), inayosema kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa huru na hiari kwa mtu binafsi na shughuli za uendeshaji zitakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi.

Alisema anatambua kulikuwa na mjadala mzito wa kupata maoni ya wadau kuhusu suala la mabadiliko ya mitaala ya elimu ambalo lilijitokeza na serikali katika kujadiliana wamelizungumza vya kutosha.

"Wakati maoni hayo yakiendelea kutolewa tafakuri, niwasihi mwendelee kuwapatia mafunzo ya dini watoto kupitia madrasa, shule zisizo za kiserikali, wakati haya yakipatiwa ufumbuzi," aliomba.

Alisema mwaka huu Ramadhan ilikutana na Kwaresma, ambazo ni funga mbili katika kipindi kimoja. Alisema hiyo ni baraka ya pekee na kwamba ana imani katika funga hizo, wote waliomba amani na utulivu na Mungu atayaitikia.

"Mshikamano na mashirikiano (ushirikiano) yetu (wetu) ndivyo vinavyoendeleza amani. Wito wangu kwa Watanzania wote ni kuendeleza kuishi kwa maelewano na kupendana, tuzidi kuwa kitu kimoja," alisema.

Akizungumza mara baada ya kupewa nafasi na Rais, Mbowe alisema ana uhakika mfungo wao ulikuwa na baraka kubwa kwa nchi na wamejiombea pamoja na taifa.

"Ninawaombea kheri kwa Mwenyezi Mungu yale yote mliyofanya ya kheri katika mwezi Mtukufu yakaendelee kuwa ya kheri kila siku iendayo kwa Mungu, tukajenge taifa la watu wanaopendana na wanaoheshimiana na wanaoshikamana," alisema.

Awali, katika salamu zake wakati wa swala ya Eid El- Fitr iliyofanyika kitaifa katika msikiti wa Mfalme Mohamed VI, Kinondoni, Dar es Salaam, na kuhudhuriwa na Rais Samia, Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir, pamoja na mambo mengine, alikemea ufisadi, akihimiza jamii kulinda maadili, umoja na mshikamano. Pia aliomba viongozi wa serikali na wadau kusaidia upatikanaji wa darubini ya kukusanya taarifa za mwandamo wa mwezi ili kuimarisha uhakika wa taarifa.

"Tunashukuru mabalozi, mawaziri na watu wenye uwezo mliopo hapa, kuna chombo tunakihitaji cha kutazamia mwezi, wenzetu Kenya na Zanzibar wanavyo vifaa hivi, kwa hiyo na sisi tunaomba jambo hili mtusaidie kunyoosha mkono ili kufanikisha," aliomba Mufti akifunga hotuba yake.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akitoka kwenye swala ya Eid El-Fitr, katika Msikiti Mkuu wa BAKWATA (Mfalme Mohamed VI ulioko Kinondoni, Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Maadili yatikisa sherehe za Eid

**Na Romana Mallya**

VIONGOZI wa dini na serikali, wamehimiza kasi ya vita dhidi ya vitendo vya ukiukwaji wa maadili vikiwamo ushoga, usagaji na ndoa za jinsia moja, ambavyo vimezidi kuota mizizi nchini.

Waliyasema hayo katika ibada na mabaraza ya Sikukuu ya Eid el Fitr jana katika maeneo mbalimbali. Sherehe za Eid el Fitr kitaifa zilifanyika jijini Dar Es Salaam na mgeni rasmi alikuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Rais Samia alihimiza utunzaji wa maadili huku akisema hivi sasa wanashuhudia ulimwengu ukikumbwa na wimbi wa utamaduni wa nchi zingine, kusambazwa maeneo mengine huku akiwataka wazazi na vijana wajitathmini kwa kuwa yako ya kuigwa ambayo yatawapa maendeleo na ustaarabu na ambayo hayawahusu, hivyo ni vyema wakawaachia wenyewe.

"Wazee wetu walituambia mwacha asili ni jahili (jitu jinga lisilo jitambua),tunapoacha asili yetu, tunaingia kwenye ujinga na kutojitambua na unapokuwa mjinga na hujitambui, ni rahisi mtu mwingine kukuchota mawazo na kukubadilisha anavyotaka.

"Tukiacha watoto wetu, sisi wazazi tukiacha asili yetu na kufanya watoto wetu wasikue kuendana na asili zetu, tunatengeneza majahili ambao watakwenda kubadilisha akili watoke na waelekee kwenye huo mwelekeo mwingine.

"Niwaombe sana wazazi wenzangu, tukamate wajibu wetu tuliopewa na Mungu, wakukuza vyema watoto wetu kuwa na maadili mazuri, tunaambiwa tutakwenda kuulizwa, ulikuzaje mtoto wako? Lakini wazazi wetu hawa hawa, walisema mkataa kwao ni mtumwa.

"Tunapowaachia watoto wetu kuzama kwenye tamaduni za watu wengine na kukataa za kwao, wanakwenda kuwa watumwa wa tamaduni nyingine, wanakwenda kutumia hivyo hivyo huko wanakojielekeza. "Niombe sana wazazi wenzagu, tusimame vyema, kuna usasa ninatambua, na tunaona ndio maendeleo na ustaarabu, lakini tutapata maendeleo zaidi na ustaarabu mkubwa zaidi tutakapokwenda na usasa ule kwa kuendana na tamaduni zetu," alisema.

Aliwaomba wazazi wasikwepe majukumu, wawatunze watoto vile wao walivyotunzwa.

"Sisi tulitunzwa. Leo tunaitwa bibi, mama. Sasa sijui tunatetereka wapi kutunza wanaotuita mama na bibi? Twendeni kila mtu awajibike, kwa upande wake, tuokoe umati huu wa kitanzania tulionao, usiharibiwe na usipotoshwe.

Alisema Shekhe Nuhu Mruma (Katibu Mkuu wa BAKWATA) amesema kwamba, taasisi ya kwanza ya kuchunga maadili ni familia na kwamba mama anapomsaidia mtoto kwenda kwenye huo usasa, atafakari mara tatu.

"Humpendi, unamharibu, niwaombe wazazi wenzangu twende tukafanye hivyo. Nitoe wito kwa taasisi za kidini na wazazi wenzangu, tujidhatiti sana katika suala hili, kwa kukemea na kuzidisha mafunzo, tubuni mbinu za kukabiliana na mmomonyoko wa maadili wa usasa tulionao ili tuweze kutoa mafunzo kwa watoto wetu.

"Tubuni mbinu kwa usasa huu huu tulionao tunaweza, nitoe mfano niliona klipu ya askari mmoja wa polisi anawaimbisha watoto, wa pili nadhani nilimwona Waziri wa Maendeleo ya Jamii, naye kalirudia, baada ya hapo sijalisikia tena kusemwa wala kusikia watoto wanaimba popote.

"Wanawaambia akikugusa hapa sema don't touch (usiguse), watoto wanaimba, hiyo ndiyo mbinu ya kisasa, pale pale shuleni walipo, pale pale unapowapata waimbishe hiyo don't touch, mtoto atakua nayo, kwamba maeneo haya nisiguswe, lakini hatuwaambii yanapita, unakuja kushtuka mtoto ameshaharibikiwa," alisema.

Rais Samia alisema mtoto wa kike akiharibika na dunia ikishampiga kisawa sawa atakaa kitako atatulia anakuwa mwanamke yule yule, lakini wa kiume mzazi huwa na kazi ya kumrudisha na si rahisi.

"Niwaombe wanawake wenzangu mnaozaa, na wanaume mnaotusaidia kuzaa, twendeni tukawajibike kulinda watoto wetu, hii ndio hazina yetu na rasilimali yetu. Tunapokaa kwenye jukwaa tukisema mmomonyoko wa maadili hakuna anayechukua hatua, tutafikia kule kule taifa ambalo tunaliimbia," alisema.

**ARDHI NA MALI BAKWATA**

Kuhusu milki za ardhi na mali za BAKWATA aliloombwa na Baraza Rais Samia alisema alipokabidhiwa kiti mtu wa kwanza aliyemwombea alikuwa ni Mufti ambaye alifika kwake akiwa na faili lenye changamoto za mali na aliyokuta ndani hayasemeki.

"Basi kwa sababu ni kiongozi wa nchi Suluhu lazima nitafute suluhu ya changamoto zinazotukabili, ninalibeba nitakwenda nalo, lakini ni gumu kidogo kwa sababu ukiletewa tatizo ambalo imetengenezwa na wale waliokuletea, utatuzi wake unakuwa mgumu kidogo, lakini tutakwenda nalo," alisema.

Pia alizikumbusha taasisi zinazohudumia mahujaji kuendelea kutoa huduma nzuri na kuwahimiza waislamu wenye uwezo wa kukamilisha nguzo ya tano ya kiislam kutumia fursa wanazopewa kwa kuwa cha kushangaza hata nusu wamekuwa hawafiki na wanapouliza wanasema watu hawana uwezo.

Awali, Katibu Mkuu Baraza la Maaskofu Kanisa Katoliki Tanzania (TEC), Padri Charles Kitima, akitoa salamu kwa niaba ya waumini wa dini mbalimbali aliwaomba masheikh kuendelea kuiombea nchi na viongozi

wa serikali ili kuenzi uhuru wa dini.

Salamu za BAKWATA taifa zilizotolewa na Katibu Mkuu wake, Alhaji Mruma, alisema hivi karibuni kumeibuka taarifa kupitia majukwaa mbalimbali kuhusu kukidhiri mmomonyoko wa maadili katika taifa, ambapo endapo hazitadhibitiwa kasi hiyo, wataharibikiwa zaidi.

HABARI KITAIFA

# Mwinyi aonya rushwa, uvunjifu wa amani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS Wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, ameitaka jamii kuendeleza maadili ili kujiepusha na vitendo viovu vikiwamo uvunjifu wa amani, udhalilishaji, rushwa, ubadhirifu na dhuluma.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana katika Baraza la Eid el Fitr alipowahutubia wananchi kwenye ukumbi wa Shekhe Idris Abdul Wakil, Kikwajuni, Mjini Magharibi, Unguja.

Pia aliwataka wananchi kuendelea kuheshimiana, kutii sheria za nchi, kuwa waadilifu, kushirikiana na kuiendeleza amani iliyopo kwa umoja na mshikamano.

Alisema kwa nyakati tofauti viongozi wa dini wamekuwa wakiisisitiza jamii kuhusu umuhimu wa kuendeleza maadili ili kuwa na jamii yenye maadili mema lakini bado suala la kuporomaoka kwa maadili linaitesa jamii na kuchangia kuzorotesha juhudi za maendeleo kwenye ustawi wa jamii.

Pia aliitaka jamii kuendelea kupiga vita mambo yasiyoendana na maadili, mila, silka na utamaduni wa Wazanzibari ili kupata kizazi chema.

"Tuendelee kushirikiana katika kuyapiga vita mambo haya. Hayaendani na maadili mema, silka na utamaduni tulioachiwa na wazee wetu," alisisitiza.

Kuhusu malezi, Dk. Mwinyi aliwataka wazazi, walezi na wazee kuhakikisha wanasimamia malezi ya watoto wao ili wawe waumini bora na raia wema kwa nchi pamoja na kuwasimamia kupata haki yao ya elimu ikiwamo elimu ya dini na kulinda usalama wao dhidi ya mambo yanayoweza kuwadhuru.

Sambamba na hayo, aliwahimiza wazazi na walezi kuzingatia usalama wa watoto wao hasa wakati huu wa sikukuu kwa sababu ni wajibu wao kuwasimamia na kuhakikisha wako salama dhidi ya mambo yote yanayoweza kuharibu furaha na amani yao pamoja na wazazi wao.

"Wajibu huu tuubebe sote kwa kuhakikisha watoto wetu wanatoka majumbani na wanarejea wakiwa salama.

Katika hatua nyingine, Dk. Mwinyi alisema serikali yake itaendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi mbalimbali zinazowahudumia mahujaji wanaokwenda Makka, Saudi Arabia kutekeleza ibada ya Hijja, baada ya kukamika kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Alisema serikali kupitia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, itaendelea kufanya kazi kwa ushirikino na taasisi hizo ili kuzifanyia kazi changamoto zinazowasababishia usumbufu waumini wanaohitaji kwenda Hijja.

Mapema asubuhi, Dk. Mwinyi alijumuika na waumini wa dini ya Kiislamu kwenye sala ya Eid el Fitr iliyofanyika katika msikiti wa Masjid Zinjibar, Kiembesamaki nje kidogo ya Zanzibar.

Kwenye hafla ya Baraza la Eid, viongozi mbalimbali wa serikali na siasa walihudhuria wakiwemo marais wastaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Abeid Karume, Dk. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid na Mufti wa Zanzibar, Shekhe Saleh Omar Kabi.

Wengine ni Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Shaaban, Mwenza wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Hafidh Ameir, na Mawaziri na Naibu mawaziri na viongozi wengine wastaafu wa serikali.



RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaj Dk.Hussein Ali Mwinyi akihutubia katika Baraza la Eid El Fitr liliIofanyika katika ukumbi wa Shekhe Idrissa Abdulwakil Kikwajuni Wilaya ya Mjini Unguja Jijini Zanzibar jana, baada ya kumalizika kwa mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani. **PICHA: IKULU**

# Spika awaangukia viongozi dini malezi, maadili vijana

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amesema serikali itaendelea kuwategemea viongozi wa dini katika kuwaimarisha vijana kimaadili na mienendo yao ili kuwaepusha na vitendo viovu.

Amesema hayo wakati akishiriki Iftari na ugawaji wa futari kwa yatima na wajane iliyoambatana na mashindano ya kusoma Quran iliyofanyika katika Msikiti Mkuu wa Gadafi jijini hapa.

Dk. Tulia alisema serikali inawategemea viongozi wa dini katika maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye kuimarisha mwenendo na vitendo viovu vinavyofanywa na vijana ikiwamo dhambi ya ushoga, usagaji na ndoa ya jinsia moja.

Spika aliwataka waumini wa dini hiyo wenye vipato kuendelea kutoa sadaka kwa wenye uhitaji kwa kuwa kundi hilo ambalo ni la mwisho kimaisha mara nyingi limekuwa likisahaulika. "Ninawaomba moyo huu mlioonyesha kwa vitendo kwa mwezi mtukufu wa Ramadhani ambao mmewasaidia watu wasio na uwezo katika kuwapatia mahitaji yao ya kila siku, mwendeleze hata baada ya Ramadhani," alisema.

Mkuu wa Mkoa huo, Rosemary Senyamule, aliwataka waumini kudumisha amani na kujiepusha na vitendo visivyompendeza Mungu, ambavyo vimekuwa vikileta hasara kwa taifa na jamii kwa ujumla.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, aliwataka viongozi wa dini kudumisha ushirikiano na serikali ili kuwafikia wenye uhitaji kwa ajili ya kuwasaidia mahitaji mbalimbali ya kiroho na kimwili.

Mavunde ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Dodoma, alisema kuwa suala la kuwasaidia watu wenye uhitaji haliko kwenye upande wa serikali, bali ni la Watanzania wote.

Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, alisema wataendelea kutoa elimu kuanzia ngazi ya chini ili kuwajenga kiimani waumini ili kupata vijana watakaokuwa na maadili yanayokubalika kwenye jamii.

Alisema viongozi wa dini wana wajibu mkubwa wa kuhakikisha wanashirikiana na serikali katika kuwaelimisha vijana ili wajiepusha na vitendo viovu.

# Waislamu watakiwa kuishi matendo mema

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SHEKHE wa Mkoa wa Mwanza, Hassan Kabeke, amewataka waumini wa dini ya Kiislamu, kuishi matendo mema kama ilivyokuwa katika kipindi cha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Alisema hayo jana jijini hapa, wakati wa sherehe za Eid El Fitr zilizofanyika katika uwanja wa Nyamagana, zilizohudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Mkuu wa Mkoa, Adam Malima.

Shekhe Kabeke alisema katika kipindi cha mfungo wa Ramadhani, wameshuhudia waislamu wakishiriki katika matendo mbalimbali ya huruma ikiwa ni pamoja na kuwasaidia wasiojiweza pamoja na kuishi katika matendo mema.

Alisema mwezi huo unawafundisha na kuwaongoza Waislamu wote kwa kuwapa mwelekeo ambao wanatakiwa kuufuata katika kipindi chote cha maisha yao ili kumpendeza Mwenyezi Mungu.

"Mwenyezi Mungu hayuko Ramadhan tu. Yupo hadi nje ya mwezi huu Mtukufu, hivyo tuendelee kukutana misikitini, kutenda matendo mema, kuwasaidia wasiojiweza ili tuzidi kusogea karibu kwa Mwenyezi Mungu na kumpenda," alisema.

Pia aliwataka Waislamu kuendelea kudumisha undugu na waumini wa madhehebu mengine kwa lengo la kuendeleza amani, upendo na mshikamano.

"Ramadhani ya 1444 imekuwa ya tofauti kutokana na kuwa katika mfungo kwa Ijumaa tano, tumepata swala za Ijumaa tano jambo ambalo ni nadra kutokea, hivyo tunatakiwa kuendelea kumshukuru Mungu kwa kuacha mambo yote machafu," alisisitiza.

Akizungumzia suala la malezi, Sheikh Kabeke alisema kila mtu kwenye familia anatakiwa kutimiza wajibu wake kuhakikisha watoto wanatunzwa na kulindwa na kundi hilo linafuata mafundisho na kujiepusha na makundi mabaya.

Mkuu wa Mkoa, Adam Malima, aliwataka wazazi kukaa na watoto wao na kuhakikisha wanawafundisha na kuwakumbusha suala zima la maadili sambamba na kuwa na utaratibu wa kuwauliza watokapo shule kuhusu hali ilivyokuwa shuleni ili kupata taraifa zao mara kwa mara.

"Kuna shule nyingine zimepewa wasimamizi ambao wao wenyewe ndio wanaofanya vitendo hivyo, mtoto anaweza kurudi nyumbani na kushindwa kusema kutokana na vitisho na woga, walimu hawa wanakaa na watoto muda mrefu zaidi, hivyo mkigundua jambo lolote leteni tulishughulikie, hatupo tayari kuvumilia vitendo viovu," alisema.

Alisema serikali haiko tayari kuvumilia vitendo vya kikatili vinavyoharibu taifa kutokana na tamaduni mbaya kutoka nje.

Mkuu wa Mkoa ameyaomba madhehebu ya dini kila mmoja kwa imani yake, kuungana kupinga vitendo hivyo.

Akisoma risala ya baraza hilo, Katibu wa BAKWATA Mkoa wa Mwanza, Ramadhani Chanila, alisema baraza hilo linaendelea kutekeleza maelekezo yake ngazi ya taifa ya kupinga vitendo vinavyoenda kinyume cha maadili ya dini na taifa ikiwamo mapenzi ya jinsia moja, ulawiti, ukatili wa kijinsia, ubakaji na matendo mengi yasiyofaa kwenye jamii.

Aisema baadhi ya matendo yanajitokeza kutokana na watu wengi kujikita zaidi katika shughuli za utafutaji na kuwaacha watoto wakilelewa na watu ambao si salama kwao na kusababisha wanatumbukia katika matendo yasiyofaa.

MAKALA MAALUM

# Mchechu na njozi ya mageuzi taasisi na mashirika ya umma

## •Ni katika kutekeleza amri ya Rais kuyafumua na kuyafuta

Na Mwandishi Wetu

MASHIRIKA ya umma yaliyopata hasara nilishasema mara kadhaa mashirika haya yafanyiwe tathimini. Kufikia hapa tulipofika kuna mashirika hayafai kuwapo, mashirika mengine hayajawahi kufanya kazi ikawa na positive impact (matokeo chanya).

"Haya mashirika yanakula tu fedha serikalini yenyewe hayaleti lakini kila mwaka bajeti ya mashirika iko hapo. Yafanyieni tathmini, yanayofaa yawapo ambayo hayafai yafutwe."

Hiyo ilikuwa kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoitoa baada ya kupokea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na ile ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa mwaka wa fedha wa 2021/22. Ripoti ya CAG ilibainisha kuna mashirika ya umma ya kibiashara ambayo katika mwaka huo, yalipata hasara ya mabilioni ya shilingi.

Ripoti hiyo, kwa kiasi kikubwa, ilionekana kumkera Rais mpaka kufikia kutoa maagizo kwa Katibu Mkuu Kiongozi na wasaidizi wake kufanya tathmini ya mashirika hayo na kutoa ripoti ili kupunguza mzigo kwa serikali wa kutoa ruzuku kila mwaka kwa mashirika yasiyo tija.

Rais alitoa mfano wa Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC) ambalo alisema limekuwapo miaka mingi lakini halijaonyesha mchango wake kwa maendeleo ya nchi. Shirika lingine ni la Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL) ambalo alisema badala ya kufanya biashara ya simu, linabaki na jukumu la kuendesha mkongo wa taifa wa mawasiliano.

**KAZI IMEANZA**

Kutokana na agizo hilo la Rais Samia, inaonyesha wazi kwamba utekelezaji umeanza. Hiyo ni baada ya wiki hii Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu kuitisha mkutano wa siku mbili wa wenyeviti wa bodi na watendaji wakuu wa mashirika ya umma, yanayojiendesha kibiashara na yale yasiyojiendesha kibishara.

Kaulimbiu ya mkutano huo uliofanyika jijini Dar es Salaam ilikuwa: 'Kuimarisha Usimamizi na Uendeshaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma, Kuelekea Uwekezaji Wenye Tija kwa Taifa'.



Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu, akizungumza katika mkutano na wakuu wa taasisi na mashirika ya umma hivi karibuni. **PICHA: MAKTABA**

Mchechu aliteuliwa hivi karibuni kushika wadhifa huo baada ya kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa vipindi viwili tofauti. Chini ya uongozi wake NHC, alifanya mageuzi makubwa na kulifanya shirika kupata maendeleo na kuwa la mfano. Kabla, shirika hilo lilikuwa katika hali mbaya licha ya kuwa na mali nyingi zikiwamo nyumba za kupangisha kila kona ya Tanzania.

Miongoni mwa mambo yaliyofanyika ni kufanya mabadiliko ya muundo wa shirika, kukusanya madeni sugu kutoka kwa wapangaji zikiwamo taasisi za serikali na kuisuka upya menejimenti kwa kuondoa iliyokuwapo na kuingiza timu mpya.

Pia ilianzishwa miradi ya ujenzi wa nyumba za kupangisha na kuuza pamoja na majengo makubwa ya kibiashara. Yote hayo yalifanyika kutokana na mpango mkakati uliokuwa umeandaliwa ili kuleta mageuzi yaliyokusudiwa.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, alibainisha kuwa ofisi yake inafanyia kazi maagizo ya Rais kuzichukulia hatua taasisi na mashirika ya umma ambayo yanajiendesha kwa hasara ikiwamo kuyafuta. Alisema utekelezaji huo uko katika hatua nzuri na taarifa itawasilishwa muda si mrefu.

Pia alisema mashirika na taasisi ambazo zilikuwa zinatoa gawio na kupitia ripoti ya CAG zilibainika hazipati faida, zinafanyiwa uchunguzi ili kuangalia sababu ni nini. Alisema huenda tatizo ni mtaji, hivyo wataangalia kwa kina. Kwa wale waliopewa dhamana ya kuongoza taasisi hizo, wale wanaolegalega, walikumbushwa kujirekebisha, vinginevyo watakumbwa na 'fagilo la chuma'.

"Suala la Rais kufanya mabadiliko ni jambo ambalo linatekelezeka na liko 'serious' (makini) na yeye (Rais Samia) yuko 'serious'. Kama mtu hajajipanga vizuri kuna Watanzania wengine wanaweza kuendesha mashirika hayo," alibainisha.

**NINI KIKWAZO?**

Mchechu alianika mambo mambo manne yanayokwamisha ufanisi na utendaji wa mashirika na taasisi za umma, kubwa likiwa kukosekana kwa maono ya muda mrefu kwa watendaji. Viongozi wengi, alisema hawajui wanataka nini na nini kifanyike na wanakwenda wapi.

Sababu ya pili, ni kukosekana kwa usimamizi thabiti hali ambayo inasababisha uzembe na ucheleweshaji wa kutotimiza wajibu kwa watendaji huku jambo la tatu likiwa tatu ni aina ya uongozi uliopo kama una ufanisi au hauna ufanisi. Sababu ya nne ni kukosekana kwa mawasiliano kati ya viongozi wa bodi na watendaji wa taasisi.

Kutokana na kuwapo mamb hayo, alisema: Tuna wajibu wa kusimamia. Nini tunakitaka kwenye taasisi wajibu ni wetu. Wajibu wa kuwawezesha kimtaji ni wetu na kubadilisha baadhi ya sheria zinazowafunga miguu wanashindwa hata kukimbia au kutimiza malengo yao ni wetu.

**RIPOTI YA CAG**

Kuhusu ripoti ya CAG, Mchechu ameyaagiza mashirika na taasisi za umma, kujibu kwa wakati na kutekelezwa na kufungwa kwa hoja zote za ukaguzi za ndani na za nje zilizoibuliwa. Alisema mashirika mengi yamefanya vizuri kupitia ripoti ya CAG isipokuwa kumekuwa na kasoro ambazo zinapaswa kufanyiwa kazi.

"Yasemeeni mashirika, taasisi za umma hata baada ya kufanyiwa ukaguzi na CAG akishatia saini mnaweza kuzungumza. Msikae kimya, ukikaa kimya na kuna mazuri ambayo yamefanyika, jamii haiwezi kufahamu isipokuwa upungufu unaobainika kwenye ripoti ya mwisho ya CAG," alisema.

Alibainisha baadhi ya hoja zilizojitokeza kwenye ukaguzi wa ndani na nje za mashirika na taasisi za umma ni utendaji dhaifu wa kifedha unaosababisha mashirika kuendelea kupata hasara, kupungua kwa mapato ikilinganishwa na mwenendo wa matumizi.

"Hasara hii kwa kiasi kikubwa zinachangiwa zaidi na utendaji duni, ukosefu wa vyanzo vya kutosha na imara vya mapato na udhaifu katika usimamizi wa matumizi na mapato, ufanisi mdogo katika kuimarisha mazingira ya biashara, kuchelewa kukamilika kwa miradi, kuchelewa kulipa hati za madai, hivyo kusababisha kulipa riba kubwa za adhabu," alibainisha.

Pia alisema chanzo cha kuwapo kasoro hizo ni udhaifu katika udhibiti wa ndani, rasilimali watu na mifumo ya utawala unaochangiwa na kutokuwapo kwa sera ya udhibiti wa udanganyifu na taratibu za kuzuia vihatarishi katika mashirika na kutokuwasilisha makato ya kisheria.

Sababu zingine ni upungufu katika usimamizi wa mapato na bajeti ambako umesababisha kukusanya mapato nje ya mfumo wa kielektroniki (GePG), ukusanyaji hafifu wa mapato kutoka vyanzo vya ndani na taasisi zinazotoa mikopo kutokuwa na mifumo thabiti ya ufuatiliaji na usimamizi wa mikopo. Eneo linguine linalosababisha kuwapo kwa taarifa mbaya kutokana na ripoti za CAG ni udhaifu katika usimamizi wa ununuzi na mikataba.

"Hoja za ukaguzi kutotekelezwa kwa muda mrefu na zingine kujirudiarudia, taasisi kutokutekeleza hoja za ukaguzi kwa muda mrefu na baadhi ya hoja kubwa na za msingi kujirudia kila mwaka ni tatizo kubwa ndani ya mashirika na taasisi za umma," alisema.

**KIDOLE MAMLAKA ZA MAJI**

Kilio cha wananchi kuhusu huduma za maji safi na salama, ikiwamo upungufu wa maji sehemu nyingi nchini, kimekuwa kikubwa hali ambayo Msajili huyo alizinyooshea kidole mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira.

Licha ya upungufu wa maji, alizinyooshea kidole kuhusu kiwango kisichoridhisha cha urejeshaji wa madeni, ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya maji.

Alisema taasisi hizo, nyingi zina madeni ambayo kwa ujumla wake yamefikia Sh. trilioni 1.1.

**MAGEUZI MAKUBWA**

Mchechu aliweka bayana kuwa mageuzi makubwa ndani ya mashirika na taasisi za umma yanakuja. Alisema mageuzi yatakayofanyika ndani ya taasisi hizo ni pamoja na namna ya kuwapata viongozi. Alisema zipo taasisi zinazotakiwa kujiendesha ili kutokuwa mzigo kwa serikali.

Sambamba na hayo, mambo mengine ili kufikia melengo ya taasisi kujiendesha kwa tija pamoja na kuwa na mpango mkakati wa miaka 10, kupitia upya miundo ya taasisi, kujenga uwezo kwa watumishi, kuajiri na kuhamisha wenye ujuzi na sifa, kufanya mabadiliko ya sheria, kuimarisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi hadi Sh. trilioni 1.2 ifikapo mwaka 2025/26.

"Na sisi wenyewe (Ofisi ya Msajili) tunafanya mageuzi ya ndani ili kumudu huu wajibu. Lakini tunataka na taasisi nazo zitangulie mbele kufanya mageuzi kabla hatujamaliza," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Wastaafu polisi walia mapunjo ya mafao

**Na Romana Mallya**

BAADHI ya askari wastaafu wa Jeshi la Polisi, wamelalamikia kuwapo kwa mapunjo ya mafao ya kustaafu, fedha za safari na mizigo ambazo wamesema wako waliozisotea kwa miaka miwili bila mafanikio yoyote.

Nipashe ilipomtafuta juzi Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) David Misime, ili kuzungumzia suala hilo, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo ambalo alisema linaendelea kushughulikiwa.

Akizungumza mwishoni mwa wiki kwenye ofisi za gazeti hili, Mikocheni, Dar es Salaam, kwa niaba ya wenzake, Sajini Taji mstaafu wa jeshi hilo, Thomas Mlango mwenye namba E2704, alisema baada ya kustaafu yeye na wenzake, baadhi yao wamejikuta wakipunjwa pensheni zao.

Mlango alisema alikuwa akifanya kazi katika Mkoa wa Kipolisi Ilala, Dar es Salaam na alistaafu Machi 14, mwaka jana.

"Wako waliopunjwa pensheni zao, wengine fedha za mizigo na zile za safari pamoja na familia. Binafsi fedha za safari na mizigo ninadai Sh. milioni nne.

"Mafao yamepunjwa, nilipigiwa hesabu kwa kutumia kikokotoo cha zamani lakini badala ya kupata zaidi ya Sh. milioni 47, nimeambulia Sh. milioni 32. Nilipofuatilia kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), niliambiwa kiasi nilichopewa ndiyo michango yangu kutoka kwa mwajiri," alisema.

Mlango alisema baada ya maelezo hayo, alikwenda katika ofisi inayoshughulikia mafao ya Jeshi la Polisi na kuonana na mtu aliyemtaja (jina linahifadhiwa) na kumweleza kuhusu tatizo hilo na kujibiwa kwamba suala hilo haliwezekani kwa sababu kuna michango yake na ya mwajiri haikupelekwa PSSSF kwa wakati.

Alisema mtu huyo alimweleza kwamba ili madai yake yafanyiwe kazi, ni mpaka michango hiyo ipelekwe ndipo atakapolipwa na mfuko.

Pia alisema mtu huyo alimweleza kuwa kuna fedha ambazo Jeshi la Polisi limeomba serikalini endapo zitatoka ndipo askari hao wanaodai watalipwa.

"Nimestaafu mwaka jana, nimeshakwenda kwa mwajiri wangu mpaka nimechoka na siko peke yangu. Tuko maelfu tunaodai fedha hizi wakiwamo waliostaafu nyuma yetu mwaka 2021.

"Tuliostaafu mwaka jana (2022) hatujalipwa. Tunaomba Rais Samia Suluhu Hassan ajue kuwa kuna wastaafu wametumikia Jeshi la Polisi na kumaliza muda wao kazini, lakini hatujalipwa madai yetu," alisema.

SACP Misime alisema askari huyo aliyestaafu Machi 14, mwaka jana, kumbukumbuku zao zinaonyesha ni kweli anadai fedha ambazo ni mapunjo ya malipo ya uzeeni ambayo ameshalipwa.

"Mapunjo hayo yametokana na baadhi ya michango yake kutokuwasilishwa kwenye mfuko wa PSSSF kutokana na mifumo iliyokuwapo ambayo imerekebishwa kwa kiwango kikubwa sasa."Hili ni miongoni mwa matatizo yaliyowakumba pia wastaafu wengine na tunaishukuru serikali imeshafanya kazi kubwa ya kuwalipa mapunjo hayo," alisema Misime.

"Mfano katika mwaka wa fedha 2021/2022 kiasi cha fedha kilicholipwa wastaafu ikiwa ni mapunjo ya mshahara, kodi, michango PSSSF ni Sh. 600,000,000 kwa ajili ya wastaafu 340," aliongeza.

Alisema mwaka wa fedha 2022/23, Sh. 98,158,327.32 wamelipwa wastaafu 80 ikiwa ni mapunjo ya mishahara, kodi, michango na tozo PSSSF.

"Kwa mtiririko huo na jitihada za serikali awe na subira atalipwa kwani, serikali haijawahi kushindwa kumlipa mtu mwenye madai ya haki na yaliko kwa mujibu wa sheria," aliomba.



Askari polisi mstaafu Thomas Bonaventura, akizungumza na mwandishi wa habari wa gazeti hili, Mikocheni, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOHN BADI**

## Mwenge wazindua jengo la dharura hospitali ya mkoa

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

KIONGOZI wa mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2023, Abdallah Shaibu Kaimu, ameridhia kuzindua jengo la dharura la Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ruvuma, lililojengwa kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 630.

Kaimu alisema ameridhia kufungua jengo la kutolea Huduma za Dharura (EMD) hospitalini hapo ambalo limekamilika kwa asilimia 100. Aliwataka madaktali, wauguzi pamoja na watumishi wengine kuyatunza mazingira yote ya miundombinu ya majengo ya hospitali hiyo likiwamo jengo la dharura lililojengwa kwa gharama kubwa.

Pia aliwataka wafanye kazi kwa kuzingatia maadili ya utumishi kwa kutoa huduma bora kwa wateja wao.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Magafu Majura, alisema hospitali hiyo ni miongoni mwa 28 za rufani nchini, ikipandishwa hadhi mwaka 1964 na ina watumishi 431 wa kada mbalimbali.

Dk. Majura alisema baada ya kuwapo ongezeko kubwa la wagonjwa wanaotibiwa katika hospitali hiyo hasa wa dharura, uongozi hospitalini hapo ulianza mchakato wa kuiomba Wizara ya Afya kujengewa jengo lenye nafasi kubwa ya kutoa huduma hiyo.

# Waziri atangaza kuifuta kampuni ya mbunge uwakala wa pembejeo

**Na Thobias Mwanakatwe,**
DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe ametangaza kufuta kampuni zaidi ya 700 za mawakala wanaosambaza pembejeo za kilimo kwa wakulima ikiwamo Kinanasi Agri Ltd inayodaiwa kumilikiwa na Mbunge wa Kyela (CCM), Ally Jumbe Mlaghila, maarufu kama Kinanasi.

Uamuzi huo aliutangaza wiki hii wakati akizungumza na wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA), katika kikao kilichofanyika jijini hapa.

Bashe alisema mtu yeyote akiwa katika sekta ya kilimo lazima achague mambo mawili, kuwa mfanyabiashara anayefanya biashara kwa nidhamu kwa kutomwibia mkulima, kutoleta mambo ya bandia au atoke kwenye sekta hiyo.

"Leo tumefungia mawakala kupitia TFRA (Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania) na nikuombe mwenyekiti na menejimenti, kampuni zote zilizotangazwa leo kufungiwa na TFRA kwa sababu ya uhuni waliofanya kwenye ruzuku ya mbolea, nendeni mkafute leseni ya Pest ili mtu anaondoka kwenye biashara ya mbolea. Anaondoka pia kwenye biashara ya viuatilifu," alisema.

Bashe alisema anafahamu kuna gharama katika kutoa uamuzi lakini ni vizuri kupata maumivu ya muda mfupi ili kusafisha mtandao. Kiongozi huyo aliagiza kampuni zote zilizofutwa zitangazwe kwenye magazeti.

"Nendeni mkatoe tangazo usajili wa viuatilifu vyote vya nchi. Hii toeni muda wa miezi sita watu waanze kuvisajili upya. Sisi hatuna mamlaka ya kutoa leseni lakini tuna mamlaka ya kumpa leseni ya kuuza mbolea na viuatilifu, kwa hiyo hatuwaondoi kwenye biashara. Biashara ni nyingi nchi hii, wakafanye biashara nyingine," alisema Bashe.

Mbunge wa Kyela, Mlaghila akihojiwa na redio ya Kyela FM na taarifa kuwekwa mitandaoni, alikiri kampuni hiyo kuwa ni yake na kuwataka wananchi wake wasiwe na wasiwasi, kwa kuwa bado hajapata barua rasmi kuhusu kufungiwa kwake.

"Bado hatujapata barua rasmi lakini niwatoe wasiwasi wana Kyela hakuna kibaya kilichotokea ni serikali katika kudhibiti namna hawa wakubwa wanaosambaza mbolea walivyoshindwa kufanya kazi na mawakala.

"Hakuna shida hiyo kufungiwa ni kampuni makubwa, sisi tunaendelea na ndio maana leo kama kuna mtu ametoka hapo nenda pale kwenye kampuni yetu, utaenda kupata mbolea," alisema.

Tangazo la Aprili 16, mwaka huu, lililotolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dk. Stephan Ngailo, liliorodhesha orodha ya mawakala 721 waliofutiwa usajili wa kusambaza mbolea na kampuni ya Kinanasi AGRI Ltd, ikiwa namba 267.

Katika tangazo hilo ambalo pia limewekwa kwenye tovuti ya TFRA, miongoni mwa mawakala waliofutiwa usajili ni pamoja na kampuni hiyo ambayo imetajwa inapatikana katika kata ya Kyela, wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya.

Tangazo hilo linaeleza kuwa TFRA ilibaini ukiukwaji wa Sheria ya Mbolea Na. 9 ya mwaka 2009, uliofanywa na baadhi ya mawakala wanaosambaza na kuuza mbolea nchini.

Pamoja na uvunjifu huo wa sheria, mawakala hao ikiwamo kampuni hiyo ya mbunge huyo, zinatajwa kujihusisha na udanganyifu ambao ulikuwa na lengo la kuisababisha hasara serikali.

"Hivyo, kutokana na ukiukwaji huo wa sheria tajwa hapo juu, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania inautaarifu umma kuwa, kwa kutumia mamlaka yake kwa mujibu wa Kifungu cha 14 (1) (c) cha Sheria ya Mbolea Na. 9 ya mwaka 2009 na Kanuni ya 14(1) ya Kanuni za Mbolea za mwaka 2011, imefuta leseni za mawakala 721 zinazowaruhusu kusambaza na kuuza mbolea nchini kama orodha inavyoonyesha kwenye jedwari," tangazo hilo lilieleza.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jamii iendelee kuenzi, kuyaishi mafundisho ya Mwezi Mtukufu

**WAUMINI** wa dini ya Kiislamu, jana walisherehekea Sikukuu ya Eid el Fitr ikiwa ni kumalizika kwa mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhan, ambao ulitamatika jana. Waumini hao walijumuika katika misikiti kwa sala maalum ya sikukuu hiyo na baadaye baraza la Eid lilifanyika maeneo mbalimbali huku kitaifa likifanyika jijini Dar es Salaam na mgeni rasmi akiwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Katika sherehe hizo, waumini hao pamoja na Watanzania kwa ujumla, walihimizwa kuendeleza mema yote waliyokuwa wakiyafanya wakati wa mfungo wa Ramadhan siku 30 ambao kwa mwaka huu, uligongana na ule wa siku 40 wa Kwaresma kwa Wakristo ambao ulitamatika wiki mbili zilizopita.

Nyakati za mifungo hiyo, waumini wa dini zote hizo walifunga pamoja na kufanya matendo ya huruma kama vile kugawa vyakula na vitu vingine kwa wahitaji, kutazama wagonjwa na kujinyima mambo yasiyoendana na maadili ya imani zao kama vile ulevi, uasherati na mengine ambayo ni chukizo kwa Mwenyezi Mungu na wanadamu kwa ujumla.

Wakati wa sherehe za Eid el Fitr, viongozi mbalimbali wa dini na serikali, waliwasisitiza Waislamu na Watanzania kwa ujumla kuendeleza mema yote ambayo yalifanyika wakati wa mfungo ikiwamo kuacha vitendo viovu, kuendeleza umoja na mshikamano bila kujali itikadi wala imani zao. Kubwa zaidi, suala la uvunjifu wa maadili vikiwamo vitendo vya ushoga na usagaji na ndoa za jinsia moja, vilichukua sehemu kubwa ya mawaidha kutoka kwa viongozi hao.

Bila kificho, viongozi hao walibainisha kuwa vitendo hivyo vimezidi kuota mizizi katika jamii ya Kitanzania, hivyo ni wajibu wa kila mmoja kusimama na kukemea ili kuvikomesha.

Sambamba na rai hiyo, Rais Samia aliwakumbusha wazazi kusimama katika misingi ya malezi ya watoto kwa kuwa wamekiuka wajibu huo. Pia aliwaonya Watanzania, hususan vijana, kundi ambalo liko katika hatari kubwa ya kukumbwa na kuangamizwa na vitendo hivyo, kuacha kuiga mila na utamaduni wa kigeni ambavyo ni chanzo kikubwa cha mmomonyoko wa maadili.


Ni dhahiri kwamba wakati wa mfungo wa Ramadhan, waumini wengi walijiweka kando na masuala ya anasa kama vile matumizi ya vileo lakini baadhi yao, jana walirejea na mambo hayo huku akiingiza katika sehemu za starehe kama vile baa na kumbi za muziki. Kurejea tena katika mambo hayo, ni sawa na kuacha mambo maovu kwa muda kutokana na jambo fulani lakini baada ya kumalizika, mtu anaendelea tena.

Kutokana na mafunzo yaliyopatikana wakati wa mfungo wa Ramadhani pamoja na ule wa Kwaresma, ni vyema Watanzania wakawa na jambo la kujifunza hasa katika kuishi maisha yenye kumpendeza Mwenyezi Mungu kwa kujiepusha na tamaa, uvunjifu wa maadili ya kiimani na kijamii pamoja na kutenda mambo mema yakiwamo kuwajali wale wenye uhitaji. Mtu anaporudi na kuendelea kutenda mambo kama hayo na hata kuwa kero kwa jamii wakati wa mfungo wa Ramadhan au Kwaresma aliyaacha, ni sawa na kula matapishi yake.

Ni vyema mafundisho kuhusu matendo mema yaliyopatikana wakati wa mifungo hiyo, yawe chachu katika kuishi maisha ya kumpendeza Mungu na jamii chini ya mwamvuli wa uadilifu. Matendo hayo na kujiepusha na vitendo viovu, ndiyo njia pekee ya kuifanya jamii kuishi kwa amani, utulivu, umoja na mshikamano.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hongera Kamanda wa Polisi Morogoro kwa hatua hii

**MWANZONI** mwa mwaka 2019, aliyekuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, alitoa maelekezo kwa trafiki akiwataka kutimiza majukumu yao kikamilifu bila kumwonea mtu.

Alifikia hatua hiyo, baada kuona mwenendo wa baadhi yao kuwa kero kwa watumiaji wa barabara, kwani wamefikia hatua ya kuwaita kwa jina la 'TRA' yaani Mamlaka ya Mapato Tanzania, badala ya kutoa elimu.

Huku akionekana kutofurahishwa na mwenendo wa askari hao, IGP Sirro akasema umefika wakati kwa trafiki kutumia busara kabla ya kuchukua uamuzi wa kuandika faini, kwa kuwa wakati mwingine dereva akipewa maelekezo anakuwa balozi mzuri wa usalama barabarani.

Akaonya kuwa trafiki kinara wa kuandika faini hizo kwa madereva, leo yuko jeshini na kesho atakuwa raia wa kawaida mitaani na atakutana nao, na kwamba ni muhimu kusamehe pale ambako kunastahili.

Nilidhani kwamba kauli hiyo nzito ya IGP ingefungua ukurasa mpya kwa askari hao ambao gari likisimama mbele yao ni kukimbilia kuingiza namba za usajili kuona kama inadaiwa au la.

Lakini pia wapo baadhi ya trafiki ambao wanatuhumiwa kuwapiga madereva, jambo ambalo ninadhani si sahihi, kwani wenye jukumu la kutoa hukumu ni mamlaka nyingine inayotafsiri sheria.

Ninadhani kama wangesikiliza kauli ya Sirro, wangejikita katika kutoa elimu zaidi ili kuondokana na mtindo wa kuwaandikia madereva adhabu ambazo wakati mwingine zinazushuka ugomvu usio wa lazima.

Binafsi ninaungana na kauli aliYowahi kusema IGP Sirro kwamba, si kila kosa ni la kuandika faini, kwani ni kweli inawezekana dereva mwingine haelewi, lakini anapaswa kuelekezwa tu, ili asirudie makosa hayo.

Ingawa haijawa wazi, inawezekana hata tukio la hivi karibuni la trafiki kumpiga dereva maeneo ya Mikese mkoani Morogoro, chanzo chake kinaweza kuwa ni dereva kushindwa kuelewa jambo fulani.

Lakini nimpogeze Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamshina Msaidizi wa Polisi (ACP) Alex Mkama, kwa hatua za kinidhamu alizochukua kwa vijana wake waliohusika katika tukio hilo.

Amekaririwa na vyombo vya habari akisema amewachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwamo kuwabadilisha majukumu ya kazi askari watatu huku hatua zaidi zikiendelea kuchukuliwa dhidi yao.

Kamanda Mkama anasema miongoni mwa askari hao, yumo Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani ngazi ya wilaya, ambaye anatuhumiwa kumpiga dereva wa gari wakati akiwa kazini.

Kwa mujibu wa Kamanda huyo, Jeshi la Polisi linaongozwa na kusimamia nidhamu, haki uadilifu, na kwamba wanapoona mambo yanakwenda kinyume, wanachukua hatua.

Aidha, analaani tukio hilo, na kwamba Jeshi la Polisi linafanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali, linaendelea na uchunguzi zaidi licha ya kuwabadilishia madaraka askari hao.

Mbali na hayo, Kamanda huyo anatoa wito kwa dereva aliyepigwa aeleze kilichotokea, na kwamba kama kuna madhara mengine aliyepata, yashughulikiwe kwa mujibu wa sheria.

Kimsingi hatua hizo zilizochukuliwa zinaonyesha kuwa Kamanada huyo anataka askari watimize wajaibu kwa kufuata utaratibu wa kazi zao ambao ni wazi unalenga kuwafanya wasionekane kama adui wa raia.

Si kwamba ninaunga mkono madereva wanaofanya makosa barabarani, bali ni vyema makosa ambayo hayana msingi kwa trafiki kuchukuliwa hatua yaachwe, itolewe elimu kama ambavyo IGP Sirro aliwahi kushauri.

Ninadhani mtindo wa baadhi ya trafiki kukimbilia kuwaandika faini madereva unaweza kuwa na mchango wa matukio ya vurugu za barabarani kati yao na madereva.

Ingekuwa ni vyema matukio kama la Mikese na mengine yanayojitokeza barabarani yakachukuliwa hatua haraka kama alivyofanya Kamanda Mkama kwa askari wake, ili kulinda heshima na nidhamu ya jeshi hilo.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Baada ya mwezi mtukufu, tusirejelee maovu



Pascal Mayalla

**Sikukuu hizi zote mbili zimetanguliwa na mfungo, kwa Wakristo ni mfungo wa siku 40 za Kwaresma na Waislamu ni mfungo wa siku 30 za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Wakristo na Waislamu waliishi maisha mtakatifu na matukufu kwa kutokutenda dhambi.**

WIKI iliyopita, Wakristo walihitimisha mfungo wa Kwaresma wa siku 40 kwa kusherehekea Sikukuu ya Pasaka na jana, ndugu zetu Waislamu walihitimisha mfungo wa siku 30 za Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, kwa kusherehekea sikukuu ya Eid el Fitri.

Dini zote mbili Kuu za Tanzania, za Wakristo na Waislamu, zote zina sikukuu mbili kuu, kwa Wakristo ni sikukuu ya Krisimasi na ya Pasaka wakati kwa Waislamu ni Sikukuu ya Eid El Fitri na Iddi El Haji. Kati ya hizi sikukuu mbili za dini zote, sikukuu moja ni ya wote na sikukuu nyingine ni ya dini husika.

Kwa Wakristo, Krismasi japo ni sikukuu ya kuzaliwa Mwokozi wao Yesu Kristo pia imahesabika ni sikukuu ya wote na Pasaka ndiyo sikukuu ya Wakristo wenyewe.

Kwa Waislamu, Eid el Fitri, japo ni sikukuu ya Waislamu, pia inasherekewa na wote-Waislamu na Wakristo, halafu Eid El Haj na Maulid ndizo husherehekewa na Waislamu wenyewe.

Leo siku ya Eid Pili, na mimi nawatakia ndugu zetu Waislamu wote na Watanzania kwa ujumla, Eid Mubarak njema. Pia nimeukumbuka ule msemo wa Kiswahili wa Mwana Mkaidi Hafaidi Mpaka Siku ya Iddi na kusema la ukweli, pilau ya Eid inakolea kuliko pilau ya Krisimasi!.

Leo Eid ni siku ya kufaidi.

Sikukuu hizi zote mbili zimetanguliwa na mfungo, kwa Wakristo ni mfungo wa siku 40 za Kwaresma na Waislamu ni mfungo wa siku 30 za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Wakristo na Waislamu waliishi maisha mtakatifu na matukufu kwa kutokutenda dhambi.

Japo wakati wote wa siku 40 za mfungo wa Kwaresma, hakukuwa na kufuturisha kwa sababu mfungo wa Kikristo hufungwa kwa siri, mtu huwezi kujua. hivyo hakuna kufuturu pamoja wala kufuturisha ila jamii yote ya Wakristo si tu waliacha dhambi, bali pia walifanya matendo ya huruma, kutembelea ugonjwa, kusaidia yatima, wajane na wenye uhitaji, kusafisha makaburi na kutenda kila aina ya mema.

Vivyo hivyo, kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, funga ya Waislamu ni wazi na hata futari hutakiwa kufuturiwa nje kubarazani ili Muislamu yeyote anayepita kujumuika kufuturu pamoja, hivyo taasisi mbalimbali, benki, kampuni na hata watu binafsi walifuturisha na Waislamu nao wakati wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, walitenda mema kwa kuacha dhambi na vitendo viovu vilipungua.

Dini zote mbili zinafundisha hata baada ya kumalizika kwa mfungo, yale maisha matakatifu na matukufu yaendelee.

Kama uliacha kutenda dhambi fulani wakati wa Mwezi Mtukufu, mfano ulevi, uhuni, wizi, au wale dada zetu wa usiku na ile 'biashara' yao, hata baada ya mfungo wa Mwezi Mtukufu kumalizika, wanatakiwa wasirudie kufanya dhambi au kurejelea vitendo na badala yake kuendelea kuishi maisha matakatifu na matukufu ya bila dhambi kama enzi za Mwezi Mtukufu.

Japo Waislamu na Wakristo ni dini mbili tofauti, wote wawili ni watoto wa baba mmoja, Nabii Ibrahim au Abraham, hivyo Mungu wa Wakristo na Waislamu ni Mungu mmoja yule yule akiitwa kwa majina tu tofauti, Wakristo wakimuita Mungu Baba Mwenyezi, Waislamu wakimuita Allah Subhana Wataala.

Dini zote mbili japo zinatumia vitabu tofauti, Wakristo wakitumia Biblia Takatifu, na Waislamu wakitumia Quran Tukufu, dini zote mbili zinatumia sheria ile ile moja, sheria ya Mussa ambayo ndani ya Biblia imeshushwa kwenye kitabu cha Kumbukumbu la Torati na kwenye Quran ni kwenye kitabu cha Taurat.

Waislamu ni uzao wa mtoto wa kwanza wa Nabii Ibrahim aitwae Ismail aliyezaliwa na mjakazi wa Kimisri wa mke wa Ibrahim, Sarai, aitwae Hagir. Wakristo ni uzao wa mtoto wa pili wa Ibrahim aitwae Isaka, aliyemzaa na mkewe Sarah. Ndani ya kitabu cha Quran Tukufu, Yesu Kristo anatambulika kama Nabii Issa bin Maryam, na sifa zake zimetajwa.

Kwa hiyo kama Wakristo na Waislamu ni watoto wa baba mmoja Ibrahim na Mungu ni mmoja, Mungu Baba wa Mbinguni, na sheria ya Mungu ni sheria moja ile ile sheria ya Mussa, sisi wote Wakristo na Waislamu tunapaswa kuishi maisha matakatifu na matukufu ya kutotenda dhambi kumcha na kumpendeza Mungu wetu au Mola wetu.

**Iddi Mubarak**
**Paskali.**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Wananchi muda wa kutathmini wabunge sasa umewadia



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

**Sisi tusio na shauku ya kuingia bungeni, sisi pangu pakavu tia mchuzi, tunaotumika kuingiza watu bungeni, huenda tukaonekana malaika kwa wawaniaji wa Mjengo. Tujiandae tu, kuitikia marahaba kutoka kwa viumbe wengine.**

UKIPATA nakala ya Nipashe ya Aprili 21 mwaka huu, nikimaanisha Ijumaa iliyopita, ukafungua ukurasa wa saba, pale chini utakutana na kikaragosi cha Kabwela. Kwenye kikaragosi hicho, Kabwela anaulizwa na mshikaji wake: "Kabwela hebu nipe mipango yako ya baadaye ukishastaafu kufanya kazi."

Kabwela anamjibu: "Najitupa kwenye siasa, naweza kubahatika kuzikwa kwa mizinga." Hayo ndiyo matumaini ya Kabwela katika mustakabali mzima wa maisha yake.

Anaamini kuwa siasa ndiyo fani inayomwezesha mtu kupata heshima, hata kuzikwa kwa kupigiwa mizinga atakapokuwa ameaga dunia. Ni matamanio ya watu wengi duniani wakiwamo Watanzania.

Wengi huamini kwamba bila kuwa mbunge si rahisi kujulikana, lakini pia si rahisi kuwa na maisha mazuri ya sasa na hata baadaye na hata ukifariki dunia urithishe kizazi chako neema.

Ndiyo sababu zinapokaribia siku za uchaguzi, watu huhaha kutafuta njia na upenyo wa kuingia katika siasa na hasa kugombea uongozi na zaidi zaidi ubunge. Na akishaupata hutulia na kuona amemaliza.

Siku hazigandi, kwa kweli mbilinge mbilinge za uchaguzi zinakaribia ambapo tutashuhudia mshikemshike kila mahali watu wakikimbizana kutafuta huruma za wapiga kura ili tu waingie mjengoni.

Ni wakati ambao shikamoo kutoka kwa wazee kwenda kwa vijana zitakuwa chekwa, ni wakati ambao ukarimu na takrima zitakuwa bwerere ni wakati ambao simu zitapokewa hata bila kupigwa.

Hakika mwakani na mwaka 2025, yawezekana nchi ikaonekana yenye ukarimu mkubwa, kila Mtanzania akiwa mwema kwa mwingine, ili mradi aliyekuwa ameweka akiba yake ataitoa ili kutafutia japo kitu.

Walioko bungeni watakuwa wakitafuta kulinda viti vyao, huku walioko nje wakitaka kuvinyakua kwa namna yoyote iwayo, ili mradi watu nao waitwe waheshimiwa fulani.

Sisi tusio na shauku ya kuingia bungeni, sisi pangu pakavu tia mchuzi, tunaotumika kuingiza watu bungeni, huenda tukaonekana malaika kwa wawaniaji wa Mjengo. Tujiandae tu, kuitikia marahaba kutoka kwa viumbe wengine.

Hata hivyo, hadhari ni kwamba katika kipindi hiki kinachoishia, kilichoanza mwaka 2020, kinachoitwa cha mauzauza ya 'uchafuzi', kuna watu waliingia bungeni si kwa ridhaa ya wananchi.

Yako madai na maelezo kuwa kuna watu waliingia tu kwa hila bila kuwa na sifa za ubunge, kwa maana ya sifa na uwezo lakini pia taratibu za kivyama kukiukwa waziwazi.

Ikasemekana kuwa hivi sasa tulilo nalo ni Bunge la chama kimoja ndani ya mfumo wa vyama vingi. Kwamba eti hivi sasa mambo ya chama tawala yanapita tu kiulaini kwa kuwa wa chama kimoja ni wengi.

Yawezekana, lakini kwa tuliopata kushuhudia Bunge la mfumo wa chama kimoja enzi za kina Njelu Kasaka, Jenerali Ulimwengu, Tuntemeke Sanga, Tabitha Siwale na wengineo, tunakumbuka lilivyokuwa.

Ikumbukwe hata la vyama vingi enzi za kina Mabere Marando, Tundu Lissu, Zitto Kabwe, James Mbatia, Freeman Mbowe na wengineo, siwezi kuwataja wote hapa, lilivyokuwa. Mambo hayakupita kiulaini kama leo.

Mambo zamani yakiwa ya kutoa shilingi kwenye Bajeti mpaka Waziri atoe maelezo ya kwa nini hili liwe hivyo na kwa sababu gani hilo halikuwa hivyo. Vikao vya Bunge vikiahirishwa ili mpaka majibu yapatikane. Leo hakuna!

Ila jambo la msingi kwa Watanzania leo, ni kwamba ni vema kuangalia ni nani alifanya nini katika miaka hii mitano inayoishia ya Bunge na kuona kama anatosha kuendelea au apigwe chini.

Tutazame ni mbunge gani alifika jimboni mwake kila mara na si kutalii, bali kuangalia kero za wananchi wake na kuzitatua. Kwa sababu kuna wabunge waliamua kujitenga na watu wao huku wengine wakibagua watu wao.

Kuna wabunge wakasikika wakiwateta wapiga kura wao, eti hawa ni wabishi hivyo siwezi kuwasaidia kwa lolote. Na kweli leo ukitazama katika baadhi ya majimbo ya wabunge hao hakuna kitu ni matatizo matupu!

Wananchi, chonde chonde wabuge wa aina hiyo wasipewe muda mwingine asilani. Wapumzike wafanye mengine na si kupandia ngazi za migongo yetu na kisha kuwatelekeza. Na waliogeuza Bunge kijiwe cha milele ya maisha yao, wapumzishwe sasa waje wapya.

**Alamsiki!**

## HABARI KITAIFA

# Kenya yaisifia Tanzania usalama kazini

**Na Frank Monyo**

WATAALAM wa Wizara ya Kazi na Hifadhi ya Jamii kutoka Kenya, wamesema Tanzania imepiga hatua katika usimamizi wa masuala ya kazi hususan mifumo ya usimamizi wa usalama na afya mahali pa kazi.

Akizungumza baada ya kuhitimisha ziara katika ofisi za Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA), Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Geoffrey Kaituko, alisema nchi nyingi za Afrika zimekuwa zikitafuta uzoefu ughaibuni ilhali unapatikana katika nchi zinazowazunguka.

"Ziara yetu hapa Tanzania imekuwa ya kufana sana, tumetembelea taasisi mbalimbali chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu). Tumefurahi kwa mapokezi mazuri tuliyoyapata pamoja na mambo mazuri tuliyojifunza.

"Mara nyingi tumekuwa na mazoea ya kwenda Ulaya kujifunza mambo fulani fulani mfano kwa mambo haya ya OSHA tungetaka kwenda Ujerumani wakati hapa Tanzania kuna taasisi nzuri sana inayosimamia masuala ya usalama na afya, hivyo jambo ambalo tunatoka nalo hapa, ni lazima twende tukaanzishe taasisi kama hii," alisema Kaituko.

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Jamal Katundu, alisema ofisi hiyo imejifunza mambo mengi kupitia ziara ya wataalam hao ikiwamo walivyofanikiwa kuwezesha watu wao kupata ajira nje ya nchi na kupata fedha nyingi za kigeni.

"Saudi Arabia wana wafanyakazi zaidi ya 120,0000, Qatar zaidi ya wafanyakazi 60,000 na nchi nyingine za Kiarabu zaidi ya 40,000, hivyo nimejifunza kwamba, fedha wanayopata kutoka nje kutokana na ajira za nje ni zaidi hata ya fedha zinazotokana na mazao yao makuu ya biashara kama vile kahawa na chai.

"Nimemwelekeza mkurugenzi anayehusika na huduma za ajira aangalie ni kwa namna gani tunaweza kujifunza kutoka kwa wenzetu ili nasi tuweze kunufaika na ajira za nje ya nchi," alisema Prof. Katundu.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema ziara hiyo inafungua ukurasa mpya wa ushirikiano hususan kwenye eneo la sheria na taratibu mbalimbali za kazi baina ya OSHA Tanzania na Kenya, jambo ambalo litakuza uwekezaji pamoja na kuleta ufanisi katika utekelezaji wa sera ya soko la pamoja la Afrika Mashariki.

"Tumekuwa na mazungumzo mazuri sana, tumejifunza kutoka kwao na wamejifunza kutoka kwetu lakini tunafahamu kuwa sisi ni Jumuiya ya Afrika Mashariki, na katika jumuiya hii, kuna kitu kinaitwa Soko la Pamoja na kuna wawekezaji wa Tanzania huko Kenya na wao wapo hapa kwetu," alisema.

Mkurugenzi wa Masuala ya Usalama na Afya katika Wizara ya Kazi Kenya, Dk. Musa Nyandusi, alisema wako mbioni kuunda taasisi mahsusi kwa ajili ya kusimamia masuala ya usalama na afya ili kuendana na miongozo ya Shirika la Kazi Duniani (ILO).




Waendesha vyombo vya moto wakipita kwa taabu katika eneo la Kitunda Kati, jijini Dar es Salaam kutokana na barabara hiyo kuharibika vibaya kwa sababu ya mvua kubwa za masika kunyesha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Watumishi DART watakiwa kufanya kazi kwa bidii ili kuboresha utoaji wa huduma

**Na Joseph Mwendapole**

WATUMISHI wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) wametakiwa kufanya kazi kwa kujituma na kuongeza ubunifu zaidi ili kuwapa huduma bora ya usafiri wa umma wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Wito huo ulitolewa juzi jijini Dar es Salaam na Mtendaji Mkuu wa DART, Dk. Edwin Mhede, katika mkutano wa tisa wa wafanyakazi wa DART.

Alisisitiza kuwa utendaji kazi uliotukuka ndio kigezo cha kufanya Wakala uonekane unatekeleza majukumu yake ipasavyo.

Akizungumzia tabia za kutowajibika na kutofuata sheria na kanuni za utumishi wa umma, Mtendaji Mkuu huyo alikemea tabia ya uchelewaji kwa baadhi ya watumishi jambo ambalo linarudisha nyuma utoaji huduma bora kwa wananchi.

Dk Mhede pia aliwataka watumishi kushiriki kushiriki bila kukosa katika matukio mbalimbali ya Wakala yakiwamo yale ya michezo na mabonanza kwani ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku na kwamba kwa watumishi wa umma kila tukio rasmi ni sehemu yao ya kazi hivyo hawatakiwi kukosa.

Mbali na kuwataka kufanya kazi kwa bidii, aliwakumbusha watumishi hao kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2019 kifungu cha 298, pamoja na kanuni za utumishi wa umma Namba 444 za mwaka 2022 zinazoelekeza namna bora ya utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya kiutumishi.

Dk. Mhede alisema watumishi wa umma pia wanaongozwa na maadili ya utendaji kazi katika kuhudumia wananchi, hivyo wanapaswa kuzingatia utii kwa serikali, kuheshimu sheria,uadilifu, usawa,uwajibikaji, ubunifu na kujitahidi kutunza siri na taarifa rasmi za serikali.

Aidha, aliwata wasimamizi wa kazi na wakuu wa Idara na vitengo kuwaheshimu walioko chini yao na kuwatendea haki bila ubaguzi wa aina yoyote huku akiwataka watumishi kuheshimu ngazi za utendaji mahala pa kazi ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima.

"Tunaongozwa na falsafa ya kuweka mioyo yetu katika kazi na sio kuweka kazi katika mioyo yetu ili tuweze kupata matokeo chanya, pamoja na kuwa waaminifu, kepuka uvivu, rushwa na tabia zote zisizofaa kwa watumishi wa umma lakini pia kwa jamii ya watu waliostaarabika," alisema.

Dk. Mhede pia alitumia fursa hiyo pia kumshukuru, Rais Samia Suluhu Hassan kwa kupitisha muundo mpya wa Wakala jambo ambalo limeongeza ari ya utendaji kazi kwa watumishi wa DART.

Baadhi ya watumishi waliochangia katika kuboresha utendaji kazi wa wakala akiwemo Geofrey Mgegwa, kutoka kitengo cha uhasibu, alisema maagizo ya mtendaji mkuu ni fursa nzuri kwake na wakala kwa ujumla kwa kuwa yamewakumbusha watumishi kufanya kazi kwa bidii na kujituma jambo ambalo ndilo nguzo kubwa ya mafanikio kwa mtu mmoja mmoja na hatimaye taifa kwa ujumla.

Zebu Mtawa, ambaye ni dereva wa wakala, alisema ni jambo la busara kwa mtendaji mkuu kukaa na kuwakumbusha watumishi mambo muhimu ya kuzingatia katika utendaji kazi hivyo kufanya huduma kuendelea kuwa bora zaidi, ikizingatiwa kuwa utoaji huduma ya usafiri wa umma una changamoto nyingi.

"Binafsi nimeyapokea maelekezo ya mtendaji mkuu lakini pia niwakumbushe wenzangu kuwa mafanikio yoyote yanakuja kwa kufanya kazi kwa bidii hivyo hakuna kazi nyingine iliyobaki zaidi ya kufanya kazi ili hata imani ya Rais kwa wakala iongezeke," alisema Mtawa.

## Tabora na Mtwara vinara kwa malaria

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imetangaza mikakati kabambe ya kupunguza ugonjwa wa Malaria kwenye mikoa minne inayoongoza kwa ugonjwa huo ambayo ni Tabora, Mtwara, Shinyanga na Kagera.

Kaimu Meneja wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria wa Wizara ya Afya, Dk. Abdalah Lusasi, alisema jana jijini Dar es Salaam kuelekea Siku ya Malaria Day duniani ambayo inatarajiwa kufikia kilele Aprili 25, mwaka huu, kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam. Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Kaulimbiu ya mwaka huu ni: "Wakati wa Kutokomeza Malaria ni Sasa, Badilika, Wekeza, Tekeleza."

Alisema ugonjwa huo kitaifa umeendelea kupungua kutokana na mikakati mbalimbali kwa kuwa mwaka 2008, maambukizi yalikuwa asilimia 18.1 lakini kufikia mwaka huu yamepungua hadi kufikia asilimia 8.1.

Alitaja moja ya mkakati kuwa ni kuwafuata kwenye makazi yao watu wanaofika kwenye vituo vya afya wakapimwa na kukutwa na maammbukizi ya ugonjwa huo.

"Tutahakikisha wanaokutwa na maambukizi wanapata matibabu sahihi na tunapeleka huduma ya vipimo na matibabu kwa wananchi waishio mbali na vituo vya kutolea huduma za afya kwasababu kuna baadhi ya wananchi wanaishi maeneo ya mbali sana.

"Sisi tunataka saa 20 baada ya mtu kupata homa apate matibabu na mkakati mwingine ni kuhakikisha tunatoa hamasa kwa mikoa ambayo ugonjwa huu uko chini sana kwasababu wamejisahau kabisa kana kwamba malaria haipo. Na pia tumebaini upimaji umeshuka sana chini ya asilimia 51 sasa tunataka maeneo haya waongeze upimaji,' alisema.

Alisema mkakati mwingine wanaoendelea nao ni kuendelea kuhimiza matumizi ya vyandarua vyenye dawa kwani baadhi ya watu wameacha kuvitumia kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo imani potofu.

"Tunaelekeza nguvu sehemu yenye maambukizi mengi zaidi na moja ya hatua tutakazochukua ni kugawa vyandarua, kunyunyizia dawa, kuongeza vipimo na matibabu , tuna vipimo na dawa za kutosha nchini lakini kuna wakati wananchi hawavipati ndani ya muda kwa hiyo uhamasishaji utafanyika kuhakikisha mgonjwa akipata homa apate vipimo ndani ya muda na atibiwe kwa wakati, " alisema.

APRILI 23, 2023
Nipashe

# MAISHA

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14


## Eid Pili na wali wa mandi

## MAISHA NI NYUMBA



Ukurasa 15

Using'ang'anie muonekano wa zamani wa nyumba yako




## KATUNIKA


Ukurasa 16



# 'MASCARA' KUNOGESHA MACHO

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | 8 | 7 | 3 | 5 | 6 | 3 | 7 | 1 | 7 | 3 |
| 8 | 1 | 3 | 8 | 6 | 8 | 5 | 8 | 2 | 6 | 4 |
| 8 | 3 | 7 | 8 | 3 | 9 | 7 | 5 | 8 | 8 | 7 |
| 1 | 9 | 4 | 7 | 6 | 7 | 8 | 9 | 5 | 7 | 8 |
| 1 | 9 | 0 | 4 | 8 | 6 | 7 | 3 | 9 | 5 | 7 |
| 4 | 5 | 6 | 9 | 0 | 4 | 8 | 9 | 8 | 4 | 7 |
| 9 | 9 | 5 | 8 | 7 | 9 | 5 | 7 | 5 | 9 | 5 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| T | ■ | P | W | A | N | I |
| A | ■ | ■ | ■ | M | ■ | K |
| N | ■ | I | N | I | ■ | W |
| G | O | A | ■ | N | O | A |
| A | ■ | M | T | I | ■ | M |
| N | ■ | U | ■ | ■ | ■ | U |
| I | B | E | B | E | ■ | E |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


NOA, LAO, WAO, NZI, SHAKA, UBOSI, AKILA, NONDO, THAWABU, ASHONWE

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

MWONESHE MWALIMU NJIA ALIFIKIE GARI LAKE.



## WATOTO

# PAKA RANGI



@ A.MSAMBA

## CHEKA

SHUHUDIA jinsi mgambo walipokwenda kumkamata jamaa mmoja

**Mgambo:** Hodi, hodi
**Jamaa:** Kimya
**Mgambo:** Hodi, hodi wenye nyumbaa
**Jamaa:** We nani kwani?
**Mgambo:** Sisi mgambo
**Jamaa:** Sawa, mnataka nini?
**Mgambo:** Kuongea na wewe
**Jamaa:** Kuongea na mimi?!
**Mgambo:** Ndio
**Jamaa:** Mko wangapi?
**Mgambo:** Watatu
**Jamaa:** Kama mko watatu si muongee wenyewe...!!!

**SWALI**
Paka ana manufaa gani kwa binadamu?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Unamsomesha unaamini atakuwa mkeo?

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vimbwanga vya safu hii ya maisha ndivyo yalivyo. Wiki iliyopita nilijadili mwanamke anayejuta kwa kusababisha mumewe kukimbia nyumba na kwenda kuanzisha maisha mengine.

Wiki ijayo nitakuletea hapa mifano miwili, mama ambaye mumewe anaondoka na kurudi kwa 'ku-bip' na mwingine mwanamume analia mke kakimbia na watoto na hujui waliko.

Wakati tunasubiri vituko hivyo, leo nikumegee ndoa changa inavyompelekesha kijana, zikionyesha dalili zote kwamba huko baadaye ndoa hiyo inaweza isidumu. Ama kweli Maisha Ndivyo Yalivyo.

Msomaji wangu, wakati wengine wanazikimbia nyumba zao, huku baadhi wamezijenga kwa nguvu kubwa na kwa muda mrefu, wapo wengine wanapalilia ndoa zao changa kwa matumaini ya kuishi maisha mazuri.

Na miongoni mwa hawa, tayari visanga vimeanza wengine ndani ya mwaka mmoja tu, sintofahamu kibao. Nimeeleza mara nyingi hapa kwamba siku zote hakuna jambo linalotokea chini ya mbingu pasipo na chanzo.

Nikimaanisha kwamba, jambo hilo lina mahali limeanzia. Au lipo chimbuko na pengine upo msingi uliolichipua hata kama ni la muda mrefu kiasi gani. Tunapozidi kuchambua utanielewa.

Hebu msikie kijana huyu ambaye alinipigia simu akielezea changamoto anayokutana nayo katika ndoa yake changa yenye muda wa mwaka mmoja tu. Anasema hivi;-

Aunty, napitia changamoto kubwa kwenye ndoa yangu ambayo bado ni changa. Nilikuwa na mahusiano na binti mmoja, ikatokea akabeba mimba. Mimi na binti huyu wakati tunakutana tulikuwa dini tofauti.

Wazazi wa binti wakatulazimisha tuoane. Tena walikuwa radhi binti aegemee dini yangu nami ni Mkristo. Wazazi wa pande zote waliridhia ndoa ikafungwa. Mtoto akazaliwa maisha yakaendelea.

Kila nilipokuwa nikijaribu kumsoma mke wangu nikagundua kwamba elimu yake ya kutambua mambo ni duni. Nilipodadisi kumbe hakuwahi kupelekwa shule wakati mimi nimesoma hadi kidato cha nne.

Nikawaza kwamba kwanini nisimuendeleze ili angalau aweze kujua kusoma na kuandika. Nikakaa naye nikamshirikisha nia yangu ya kutaka ajifunze kusoma na kuandika ili upeo wa kuelewa mambo uongezeke.

Alikubali na nikaanza kumfundisha mimi mwenyewe na ndani ya mwaka mmoja akaweza kusoma kidogo na hata kuandika. Wakati nawaza kumuinua katika kiwango kingine akaanza kuwa mkali kwamba hataki tena kusoma.

Jambo hili linanipa mashaka na kunihuzunisha sana. Ningetamani nimpeleke kupata mafunzo zaidi ili baadaye anisaidie katika shughuli zangu mbalimbali. Sasa nifanyeje aunty?

Mpenzi msomaji, hivyo ndivyo anavyomaliza kijana huyo katika maongezi yake. Kwa haraka vipo vitu naviona kwa wanandoa hawa.

Kwanza, walioana kwa kulazimishwa baada ya mimba kuwa kidhibiti. Na inavyoonekana kijana hakuwa amedadisi elimu ya mwenzake. Ndio maana anajaribu kutumia nguvu kubwa kuhakikisha anainua kiwango chake cha elimu.

Pili, ijapokuwa binti alikubali na kuonyesha shauku ya kusoma, lakini anashindwa kuendelea. Pengine anaona uvivu au kwao wapo wengine hawajaenda shule kama yeye hivyo anataka afanane nao.

Na kusema kweli, zipo familia ambazo elimu ya darasani siyo tija kwao, hasa kwa watoto wa kike. Wanataka wakikua, watafute waume waolewe, basi! Hiyo ni dhana ambayo imeharibu hatma ya mabinti wengi hivyo kujikuta wakiwa ni mama wa nyumbani, kuzaa na kulea watoto.

Ni kweli kwamba kijana anaona mbele kwamba kumuelimisha mkewe kutakuwa na tija siku za usoni. Lakini kwa upande mwingine, ipo mifano mingi ambapo mwanaume anamsomesha mwenzi wake hadi kwenye ngazi ya chuo kwa ahadi ya kuoana.

Lakini mwanafunzi huyu akiwa huko shuleni au chuoni, anakutana na mtu mwingine wanaanzisha mahusiano na kujikuta anampiga teke yule aliyefungua mlango wa elimu yake.

Wapo watu ambao wamepata maumivu kwa mtindo huo na kujikuta wanachanganyikiwa. Wakati mwingine maisha hayatabiriki kwani zipo nguvu laghai huingilia kati na kuvuruga mahusiano ya watu.

Unapofikiri kwamba huyu ni wa kwangu peke yangu, kumbe yupo anayemtamani na usipokuwa makini anakuponyoka, tena mbele ya macho yako! Na maadui wakubwa katika hili ni wale watu wa karibu kabisa na wewe.

Aweza kuwa rafiki wako mpenzi, ndugu yako au jirani yako. Kumbuka, siyo kila mtu anafurahia maisha unayoishi, au familia uliyo nayo.

**Je, una maoni, kisa cha kweli? Tuma ujumbe 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# 'Forensic Audit' imalize utata matrekta ya Ursus

UTATA kuhusu madai ya kukiukwa kwa makubaliano ya mkataba wa mauzo ya matrekta kati ya kampuni ya Ursus ya Poland na wakulima au wananchi wa Tanzania, unazua maswali ambayo kama hayatajibiwa kwa haraka. Unaweza kuwa sababu ya kupunguza morali ya uzalishaji wa chakula na mazao ya biashara nchini.

Bila kumung'unya maneno, nitangulize pongezi zangu za dhati kwa Mbunge wa Viti Maalum (Vijana), Asia Halamga (CCM), aliyejivisha ujasiri wa kuwasemea wananchi wanaolalamika kupata hasara kutokana na matatizo yanayoendelea katika ukiukwaji wa mkataba huo.

Aprili 13 mwaka huu, Asia Halamga, alisema tangu wananchi hususani wa mkoa wa Manyara walipoingia mkataba na kampuni hiyo chini ya usimamizi wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), hakuna vipuri vilivyoletwa nchini kwa mwaka wa pili sasa. Kwa mujibu wa Halamga, wananchi walikubaliana na kampuni ya Ursus kwamba kwa miaka miwili wataendelea kupewa huduma ya vipuri lakini matrekta hayo yamefika kwa wakulima na hakuna vipuri.

Lakini pia nimpongeze Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kwa kusikia kilio cha Mbunge Halamga na wenzake, kuhusu matrekta hayo kuongeza umasikini kwa wananchi na kuamua kuipeleka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika mkoa wa Manyara kwenda kusikiliza, kuchunguza malalamiko na changamoto za mkataba huo na kupeleka mapendekezo yake Bungeni.

Spika Dk. Tulia, ameguswa. Anajua taabu za wakulima masikini, wanaobangaiza kutafuta walau kufikia kiwango cha maisha bora. Hiyo ni baada ya kubaini kwamba kuna umuhimu wa kamati husika kushughulikia malalamiko ya wananchi, ambayo yametolewa Bungeni na mwakilishi wao.

Ni dhahiri kwamba, Bunge litapata mrejesho kamili wa suala hilo kwa mujibu wa Spika Dk. Tulia, wakati wa kipindi cha siku sita cha majumuisho ya bajeti, kwa mujibu wa Kanuni ya 124.

Kwa namna ambavyo mkataba huo ulivyogubikwa na utata, hata baada ya kamati kuwasilisha Bungeni mapendekezo yao kutokana na walichokibaini kwa wakulima kuhusu mkataba huo, kuna haja ya kuchukua hatua zaidi kwa kwa Bunge letu kuagiza, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi, yaani 'forensic audit'.

Ndio! CAG anapaswa afanye 'forensic audit' katika mkataba huo ulioingiwa Oktoba 22, 2015, kati ya NDC na Ursus iliyojenga kiwanda cha kuunganisha matrekta hayo Kibaha, mkoani Pwani, kwa sababu kuna viashiria pia vya udanganyifu kama ambavyo malalamiko yametolewa na Mbunge Halamga.

Inaelezwa kwamba, wakulima ili kukabiliana na changamoto ya fedha za mkopo wa matrekta hayo, wanalazimika kununua na kutumia vipuri vya trekta aina ya Massey Ferguson kwa kuwa wenye matrekta hawana vipuri na wameshindwa kuvileta nchini.

Moja ya masharti ya mkataba huo, inaelezwa kwamba mkataba unawataka wawekezaji hao wanaolipwa kwa mkopo wa masharti nafuu, kujenga vituo vinane vya kukarabati matrekta na kuwa na magari ya kwenda vijijini kuhudumia matrekta ya wakulima.

Oktoba 27, 2014 huko Warsal, Poland. Rais wa Bodi ya Ursus, Karol Zarajczyk, alipokutana na Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda (wakati huo akiwa Waziri Mkuu), pamoja na wafanyabiashara wenye nia ya kuwekeza Tanzania, alisema wako tayari kutoa mafunzo kwa vijana wa Tanzania waliopo vyuoni ili waweze kuunganisha matrekta hayo, kuyafanyia ukarabati na kutengeneza vipuri vyake wakati kunapokuwa na ulazima wa kufanya hivyo, lakini je hilo linafanyika?

Kwa muktadha huo, tunataka mabadiliko ya msingi ya mkataba, kati ya Tanzania na Ursus ambayo kwa jinsi mkataba wao ulivyokaa, unapingana na mkataba mama ulioingiwa kuchukua mkopo kati ya Tanzania na Poland. Haiwezekani tukaendelea kuliacha suala hilo kuchukua suara ya kisiasa, tuwasaidie wakulima wetu kwa kuzuia wasiuziwe matrekta mabovu.

Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini.

**Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**












Sherehe ya SendOff inapendeza kama kutafanyika chaguo zuri la gauni la bi harusi mtarajiwa. Pichani ni baadhi ya magauni yanayofaa kuvaliwa siku hiyo muhimu. PICHA: PIRENTES

# MITINDO



## MINYUMBULIKO INAYOVUTIA

Ni jambo linalotaka uzoefu kutembea kwa madaha pale mwanamke anapovaa kwa mara ya kwanza.

Wengi wanashindwa kutembea vizuri hasa wakiwa kwenye mialiko ya sherehe mbalimbali kutokana na magauni hayo kuwapa shida wakati wakipiga hatua.

Endapo inahitajika hali ya kujiamini na mtazamo alisia, ni kujifunza namna ya kupiga hatua ukiwa na gauni refu linalojiachia chini.

Kuna aina tofauti ya kutembea na gauni la harusi, lazima kujifunza na kujipa uzoefu kabla ya siku ya tukio.

**JIFUNZE KUTEMBEA**

Usitembee haraka au kujitingisha Chagua gauni ambalo litakufanya utembee kwa madaha, mwendo wa pole na wenye kukupa muonekano mtulivu. Hata kama gauni limetengenezwa kwa aina tofauti ya vitambaa ni wazi unaweza kutembea kama inavyohitajika.

**Vaa viatu vinavyokutosha.**

Kama unahitaji kuwa huru na raha zaidi katika mwendo, unatakiwa kuvaa viatu vyenye visigino vya wastani.

Ni vizuri viatu vya aina hiyo vitakupa usalama zaidi na muonekano mzuri. Ukitembea mwendo wa paka yaani kupishana miguu ni wazi utapendeza zaidi.

Chagua kiatu kinachoendana na gauni

Hakikisha rangi ya gauni inaendana na kiatu unachovaa kwani itakufanya kuongeza mg'aro.

**Jifunze kutembea mwendo wa kinyonga**

Unatakiwa kujifunza kwa ufasaha kutembea mwendo wa 'kinyonga' ukipiga hatua kwa kuhesabu. Ni muhimu mtu maalum akawa anakuangalia jinsi unavyotembea ili kukufanya uwe na mwendo unaotakiwa.

**Kuwa huru na jiachie**

Unatakiwa kutulia katika siku yako hiyo muhimu, ukifanikiwa hilo kila kitu kwako kitakuwa rahisi. Usihofu kuhusu kutembea muda wote, au jinsi ya kusimama bali faya jambo hilo kama rahisi kwako na unaweza kulifanya na hapo utapata matokeo mazuri.






URMBO

Na Mary Geofrey

# 'MASCARA' KUNOGESHA MACHO



KIPODOZI cha mascara kinatumika kama kinogesho cha mvuto wa kope zako, kwa kuongeza ujazo na urefu wake.

Mascara zinakuja katika aina mbalimbali na zenye matumizi mbalimbali, zipo za kuongeza urefu wa kope, ujazo wa kope, kunyoosha na kukunja kope katika rangi tofauti,

Katika rangi zipo nyeusi, kahawia, blue, colourless na kijani.

Hata hivyo, rangi hizo inategemea na anayetumia anapendelea nini na anaenda kwenye tukio gani.

Jambo la kuzingatia ni kuzingatia kope zako zikoje na utumie mascara ipi ili kuvutia macho yako.

**Mambo ya kuzingatia**

Kama una kope fupi tafuta mascara inayoongeza urefu yaani ;lengthening mascara' ili kuongezea urefu wa nyusi zako na kuzifanya ziwe na mvuto zaidi.

ama una kope nyembamba, basi utazijaza kiasi cha kutosha kwa kutumia mascara inayoongeza ujazo, yaani 'voluptuous mascara'.

Kama una kope ndefu tumia mascara inayokunja nyusi (curling mascara) itakayozifanya kope zako ndefu zijikunje kwa madaha zaidi na mvuto zaidi.



Kama una macho yaliyo na matatizo tumia 'gentle mascara' ambazo ni maalumu kwa macho ya aina hiyo hasa wanaovaa lenzi kwa kuwa hazileti muwasho na kuvimba kwa macho.

Mascara ya rangi nyeusi huwa inatumiwa zaidi sababu inaweza kutumika katika mazingira mbalimbali na kwa macho ya rangi yoyote.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Eid Pili na wali wa mandi

JANA ilikuwa sikukuu ya Eid El-Fitri, wengi wamesherehekea kwa kula na familia zao nyumbani.

Chakula kikubwa cha sikukuu kubwa kama hii ni pilau nyama na mazagazaga mengine ili mradi tu kuwapa furaha ndugu, jamaa na marafiki.

Sasa leo kwa sababu sikuu inaendelea sio mbaya ukala mandi ya mbuzi ili kubadili ladha ya msosi.

**Mahitaji**

Nyama ya mbuzi (mbavu), mchele vikombe viwili, tangawizi vijiko viwili vya chakula

kitunguu swaumu kijiko kimoja cha chakula, mdalasini kijiko cha chai kimoja, karafuu nzima kijiko cha chai kimoja, iliki nzima kijiko kimoja cha chai, chumvi kijiko cha chai nusu, limau au ndimu

Curry powder, zafarani na kitunguu maji kimoja kikubwa.

**Jinsi ya kupika**

Chemsha nyama yako weka curry powder, limau, chumvi, tangawizi, swaumu, karafuu na mdalasini wacha ichemke hadi maji ya kwanza yakauke, weka maji mengine wacha nyama ichemke hadi iive.

Toa nyama weka katika tray, weka ile supu katika bakuli pembeni.

Ile nyama iweke kwenye oven kwa dakika 10 moto wa180 hakikisha haikauki.

Bandika sufuria jikoni kaanga vitunguu maji, weka thomu na tangawizi, hiliki na abdalasini nzima kaanga, weka ajnamoto.

Wacha vichemke lama dakika tano weka mchele ukaange halafu weka ile supu funika.

Ukishaiva weka zafarani au hata rangi ya chakula unayoipenda.

Hakikisha unaugeuza wali kabla haujaweka rangi na pia hakikisha wali hauvunjikivunjiki.

Changanya wali na zile nyama, mandi tayari kwa kuliwa.

Furahia msosi wako mtamu kwa sikuu hii unaweza kushushia na juisi, soda au kinywaji chochote pendwa.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Using'ang'anie muonekano wa zamani wa nyumba yako



## Maajabu ya tairi chakavu katika mapambo

**Restuta James**

KILA kitu kinaweza kubadilishwa na kutumiwa kubadili mwelekeo wa bustani au nyumba yako, ni kiasi cha namna mtu anavyotazama vitu.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wanaeleza kuwa kila kitu kinafaa kubadilishwa, safari hii wakizungumzia matumizi ya tairi chakavu kama moja ya zana za kubadili mwonekano wa nyumba.

Wanaeleza kuwa tairi hizo zinaweza kupakwa rangi nyeupe, nyekundu, njano, bluu, pinki, kijani au nyeusi kulingana na mapenzi ya rangi kwa mwenye nyumba.

Aidha, tairi hizo zinaweza kupakwa rangi za aina tatu na kuongeza nakshi stahiki. Hata hivyo, wanaeleza kuwa inategemea ni wapi hasa mtumiaji anapanga kuziweka kama ni chini au kuning'iniza.

Wanaeleza kuwa tairi zinaweza kutumika kama chombo cha kupandia maua nje ya ukuta, kutengeneza fasheni ya mzunguko (round about) au ngazi kwenye bustani.

Pia wanaeleza kuwa tairi zinaweza kuning'inizwa ukutani kwa kushikiliwa na msumari au kifaa kingine kitakachopatikana kwa urahisi.

Rangi zinazoshauriwa kupakwa kwenye aina hii ya pambo ni zile angavu kama pinki, njano, bluu bahari, nyekundu na nyeupe. Hii ni kwa sababu maua mengi yanatawaliwa na rangi ya kijani hivyo kupaka rangi hizo kutaongeza mwonekano mzuri zaidi.

Kwa mujibu wa wataalamu hao, si maua pekee unayoweza kupanda kwenye tairi bali unaweza kuzitumia kutengeneza bustani yako ndogo ya mboga mboga nyumbani.

**0753 333 330 Dar es Salaam**



BAADA ya miaka kadhaa ya kuishi kwenye nyumba, wengi hutamani kubadilisha muonekano.

Na mara nyingi wamiliki wengi wa nyumba hupendelea kurekebisha jengo au kununua samani mpya ambazo hutumia gharama kubwa.

Si vibaya kufanya hivyo, lakini hata pale bajeti inapokuwa ndogo unaweza kufanya maboresho hayo.

Miongoni mwa vitu ambavyo unaweza kuvitumia kubadilisha muonekano wa nyumba yako hata bila ya kutumia gharama kubwa na ikapendeza ni pamoja na namna kuchagua rangi ya ukuta.

Nyingine ni matumizi tofauti ya karatasi za ukutani na malighafi nyingine zilizotumika kutengenezea samani zako ambavyo vikitumiwa vizuri vina nafasi kubwa ya kubadilisha kabisa muonekano wa nyumba yako na kukupa wa kuvutia zaidi.

Kwa mfano kupaka rangi upya kabati la luninga, miguu ya kiti au meza, kubadili kitambaa kilichotengenezea viti au sofa,nako kunasaidia kubadilisha muonekano katika nyumba yako.

Nyingine ni kubadili vitu kidogo kidogo kama vile tai na fimbo za pazia, pazia zenyewe, zuria, mapambo ya ukutani na mengineyo.

Vipo vitu vingi ambavyo unaweza kuvifanyia marekebisho kwa gharama ndogo ndani ya nyumba yako na ukaifurahia tena na usiichoke.

Pia hata kuchagua kubadili kitu kingine unachoona unatakiwa kufanya hivyo. Kama ni foronya unatakiwa kuangalia zile zinazoendana na zilizoko kwa wakati wa sasa.

Kama vitu vyako vya ndani umevitumia kwa miaka mingi na vimepitwa na wakati na ndiyo maana huenda vinakuchosha na kuiona nyumba yako mbaya, usiikatie tamaa kwa sababu inawezekana kuirudisha katika ubora wake.


Kikubwa ni kuwa mbunifu na kuongeza kidogokidogo vionjo vinavyoendana na wakati katika nyumba yako hiyo, hata kama huna kipato kikubwa inawezekana, si lazima uweke vyote kwa pamoja, lakini kadri unavyojaaliwa unabadili cha zamani na unaweka kinachoendana na wakati wa sasa.

Utanunua pazia leo lakini siku nyingine kitu kingine na hii pia itasaidia nyumba yako kuonekana mpya kila siku.

Ni ukweli kuwa vitu vya nyumbani vinabadilika kila baada ya kipindi kifupi, zuria ulilonunua miaka mitano iliyopita, haliwezi kuendana na wakati huu.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
JANA NIMEKUWINI UMESHINDA NDANI UNAANGALIA VIDEO, SASA LEO NAKURUHUSU UKAOSHE MACHO ILA 'OLE WAKO URUDI UNAYUMBAYUMBA'
ETI MAMSAP' IKITOKEA IBILISI KANIMEZESHA WALAU GRASS MOJA JE?
SUKA ACHA USHAMBA BUANA!
KUCHORA KACHORENI KWENYE MADAFTARI YENU AU KWENYE VIWAMBAZA VYA NYUMBA ZA WAZEE WENU MSINITAFUTIE KESI ZA KUJITAKIA
TUKIFIKA BICHI WE MZEE LAZIMA TUKAKULOWANISHE UTETEMEKE BARIDI
MI'NILIPOONA DEREVA ANA KIWALAZA NIKAJUA WAZI KUWA LEO KAZI TUNAYO!
DEREVA WA DALADALA HAWEZI KUWA NA KIWALAZA HUYU NI MUHASIBU
BICHI 'KIBWAWA'
USISAHAU SIKU NILIPOKUJA KULETA KITAMBAA UMSHONEE MKE WANGU GAUNI LA SIKUKUU 'NILIVAA VIPI!'
OH! MHESHIMIWA MJEDA HAPA NILIPO 'NSHAJICHAFULIA' SIJUI KIFO CHANGU KITAKUWA CHA FLEVA GANI!
SIWEZI KUTOKA NA MWANAUME SIKU KAMA YA LEO TUKAKAE BAR TUTUMBULIANE MIJICHO KAMA TUNASUTANA
NA MIMI SIKUKUU YA LEO 'FUBA LANGU' LIMENIPIGA MARUFUKU KUTOKA NA JITU LENYE GUBU
KINACHONIONDOA SIO KODI NIMECHOKA KUELEA NIKIWA CHUMBANI KWANGU
USINITANIE NIMEACHA WATU BAR WANANISUBIRI NIMEWAAMBIA NAKUJA KUCHUKUA KODI YANGU ILI SIKUKUU YA LEO TUBEBWE NA MACHELA USINIAIBISHE
NIMEVUMILIA SIKU THERASINI SIJAGONGA 'MATINGASI' ETI LEO IBILISI KAKAA KOONI ANANIVUTIA BAR! SIJUI NIMUHURUMIE!
*KINYUNYIZO CHA LEO... ...UKWENI SIO KWENU

## HABARI PICHANI

# SHEREHE ZA EID EL FITR KATIKA PICHA



Shekhe Mkuu wa Tanzania Mufti, Abubakar Zubeir, akihutubia katika Swala ya Eid el Fitr kwenye Msikiti Mkuu wa Bakwata uliopo Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Waumini wa dini ya Kiislam, wakiwa katika Swala ya Eid el Fitr katika Msikiti Mkuu wa Bakwata uliopo Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Shekhe wa Malindi Mombasa nchini Kenya ,Saidi All Hassan (kulia) akitakiana heri ya Sikukuu ya Eid el Fitr na Ismail Dwood mkazi wa Jijini Dodoma mara baada ya swala ya Eid iliyofanyika uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Wanawake wa dini ya Kiislamu wakiswali kwenye viwanja vya msikiti mkuu wa Gadafi Dodoma katika swala la Eid el Fitr iliyofanyika jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**



Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mariam Mwinyi akifuatilia hutuba ya Baraza la Eid El Fitr, wakati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaj Dk.Hussein Ali Mwinyi akihutubia katika ukumbi wa Shekhe Idrissa Abdulwakil Kikwajuni Wilaya ya Mjini Unguja Jijini Zanzibar jana, kulia kwake ni Jamila Mwinyi na (kushoto kwake) Mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar Mama Zainab Kombo Shaib,Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Mhandisi Zena Ahmed Said. **PICHA: IKULU.**



Waumini wa dini ya Kiislam, wakitoka katika swala ya Eid el Fitri katika Msikiti Mkuu wa Bakwata uliopo Kinondoni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

MAKALA

# UWAJIBIKAJI WA VIONGOZI NCHINI UKO WAPI?



Na Magabilo Masambu

MACHI 29 Machi, 2023 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, aliwasilisha ripoti ukaguzi wa serikali kuu kwa mwaka wa fedha 2021/22 ulioishia Juni 30,2022. Utaratibu huu unafanyika kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kifungu cha 34 (1) (c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

Katika ukaguzi wake na kama ilivyo ada, aligundua ukiukwaji wa sheria, uzembe, ubadhirifu na upungufu wa kiutendaji kwa baadhi ya watumishi wa umma. Nitatoa mifano michache hapa. Mathalani, alibaini kuwa Wizara ya Afya ililipa Sh. bilioni 10.75 kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudunmia Watoto (UNICEF) kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa (ambulance) na pikipiki, huku muda wa utoaji huduma ukipangwa kuanzia mwishoni mwa Juni, 2022 hadi mwishoni mwa Agosti, 2022.

Pamoja na hayo, hadi ukaguzi unafanyika Desemba, 2022 magari hayo yalikuwa bado hayajawasilishwa.

Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB), alibaini kuwa, Wizara ya Fedha na Mipango ilihamisha tozo ya mafuta ya Sh. bilioni 330.33 moja kwa moja kwenda Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

Hata hivyo, Wizara ya Fedha na Mipango haina mamlaka ya kupeleka fedha hizo moja kwa moja kwa TARURA huku akisema kitendo hicho kilikiuka Kifungu cha 5 (4) (g) cha Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, ambacho kinaitaka RFB kuhamisha tozo ya mafuta kutoka kwenye akaunti ya mfuko.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa maelezo yake, anasema ilinunua magari matatu ya injini za zimamoto yenye thamani ya Sh. bilioni 2.98 kutoka kwa mtengenezaji asiyeruhusiwa.

Hata hivyo, malori hayo ya injini hizo za zimamoto, yalikuwa bado hayajawasilishwa hadi kufikia wakati wa ukaguzi wake Desemba, 2022 licha ya ukweli kwamba muuzaji alikuwa ameshalipwa Sh. bilioni 2.23 Februari, 2021.

Hii ni sehemu ya upungufu kati ya mengi aliyoyabaini. Lakini kwa mujibu wa CAG, katika ripoti yake anasema deni la taifa hadi Juni 30, 2022 lilikuwa Sh. bilioni 71,312.42 ikilinganishwa na Sh. bilioni 64,519.63 lililoripotiwa mwaka 2020/21.

Pamoja na taarifa hii ambayo imegusa maeneo mengi, sitaki kurudia lakini mpaka sasa hatujasikia kiongozi yeyote akijiuzulu wala kutolewa ofisini kwa tuhuma za ukiukwaji wa sheria, uzembe au ubadhirifu wa moja kwa moja. Wote wamekaa kimya.

Natambua kuwa baada ya ripoti hii, pengine ziko taratibu za kujiridhisha kama kilichosemwa na CAG ni cha kweli lakini ingependeza sana ikiwa wale wote waliyotajwa na ripoti kukaa pembembeni kupisha uchunguzi ili kutoathiri uchunguzi wenyewe, maana yake suala la uwajibikaji kwa viongozi wa nchi hii ni msamiati ambao haupo na hautakuwapo.

"Kisiasa nakiri kuwa nahusika, siwezi kukwepa kwa sababu dhamana yangu ya uwaziri inaambatana na wajibu unaonitaka nijue yanayotendeka wizarani na pia niweze kudhibiti na kuhakikisha mwenendo mwema wa Jeshi la Polisi.

Msahafu unatuhusia kwa kusema wala hatabeba mbebaji mzigo wa mtu mwingine.

Kisiasa huu ni mzigo wangu na nakubali kuubeba kwani hakuna mwingine wa kuubeba.

Kwa hiyo, Mwalimu nakuomba mambo matatu. Kwanza, naomba radhi mimi nafsi yangu, naomba radhi kwa niaba ya askari wote walipo wema.

Pili, naomba vilevile uwelewe sehemu yangu katika kosa hili. Tatu kwa fedhea hii, naomba unikubalie kujiuzulu" (Ali Hassan Mwinyi, Januari 22, 1977).

Haya ni sehemu ya maneno ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Mzee Mwinyi katika barua aliyomwandikia Rais wa Awamu ya Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere, akimwomba kujiuzulu baada ya Jeshi la polisi kuhusika na mauaji ya watu Mwanza na Shinyanga kwa tuhuma za uchawi.

Mzee Mwinyi wakati huo alikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani lakini hakutekeleza mauaji, hakuwatuma polisi wakaue, hivyo kisheria asingekuwa na hatia lakini kisiasa aliona anahusika.

Baada ya barua hii maofisa kibao walifukuzwa kazi na kustaafishwa akiwamo aliyekuwa Mkuregenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa wa wakati huo, Emilio Mzena.

Kama umewahi kusikia hospitali ya Mzena, imebeba jina la kiongozi huyo (ambaye ametangulia mbele za haki) aliyestaafishwa baada ya tukio hili.

Sasa leo viongozi wanatuhumiwa, tena kwa ubadhirifu lakini bado wako ofisini na hawana hata mpango wa kuchukua hatua. Pesa zinazopotea ambazo zingetumika kujenga maendeleo ya nchi hii.

Hospitali hazina dawa, watoto wetu shuleni kwa baadhi ya maeneo wanakaa kwenye mawe, pembejeo ziko juu, deni la taifa linaongezeka walipaji ni Watanzania wote.

Leo tuna tozo za simu mpaka pesa tunazowatumia wagonjwa au bibi na babu zetu vijijini, zinakatwa ili kutekeleza miradi ya maendeleo lakini watu wachache wanaojiona wajanja wanapiga kisha wanatamba mitaani.

Hakuna la kuwafanya na hawatawajibika. Tunapozungumzia masuala ya uwajibikaji tuna maanisha nini?

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es salaam-Tanzania**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mganga aliyempa 'dawa' mke wa adui yake



Na Adam Fungamwango

TULISHAWAHI kuwa na mada ya 'limbwata' kwenye safu hii inayowahusu baadhi ya kinadada na kinamama wasiojiamini, wanaotaka kuwadhibiti zaidi wapenzi wa waume zao kwa kutumia mbinu mbadala.

Kwa wasomaji wapya wa wale wasiojua msamiati 'limbwata', ni kuwa baadhi ya jamii za Kiafrika, inaaminika kuna dawa za kuwapumbaza wanaume watulie kwenye ndoa zao, au kuwafanya wafanye chochote kile kwa wapenzi wao.

Dawa hizi inaaminika zinatumiwa sana na baadhi ya wanawake kuwapa wanaume kwa njia mbalimbali za hila kwenye chakula, au maji ya kuoga kuwapa wanaume kwa ajili ya kuwadhibiti na 'kutiwa mikononi', wasifurukute wala kutingishika.

Jamaa anatakiwa awe kama zezeta. Kila analoambiwa akubali. Na mara nyingi baadhi ya wanawake wanafanya hivyo kwa sababu mbalimbali.

Kwanza ni kutaka udhibiti wa yeye awe peke yake, na wala mpenzi wake asiwe na hamu au kutafuta mwingine. Pili, ni uwezeshwaji. Wanachotaka kile ambacho anakipata mpenzi wake basi asilimia kubwa kama siyo 80 mpaka 90 akipate yeye, Kisiende kwa mwingine wala kisibaki kwa mpenzi wake huyo mtafutaji. Huu wote ni ubinafsi.

Ingawa mpaka sasa hakuna uthibitisho wa kisayansi unaoonyesha kuwa dawa hizo za mitishamba zinazofanya kazi ya kumpumbaza mpenzi zaidi ya dhana, lakini ukweli unabaki pale pale kuwa baadhi ya wanawake wana tabia hiyo tangu enzi na enzi na linathibitishwa na nyimbo tulizowahi kuzichapisha hapa za Mbaraka Mwinshehe Mwaruka akiwa na Super Volcano na John Simon akiwa na JKT Kimbunga Stereo.

Mbaraka akatunga wimbo unaoitwa 'Dawa ya Mapenzi' na haya ni mashairi yake.

"Kwa nini unahangaika kutafuta dawa ya mapenzi kwa waganga. Madawa yasiyopimwa yaweza kumuumiza mwezio we mama. Kwanza jiulize kwa nini hupendeki siku hizi mama. Bembeleza bwana yako muishi pamoja usitumie dawa.

Hakuna dawa kabisa ya mapenzi duniani, na sasa hiyo utafutayo ya kumuua mpenzi wako. Kwanza chungua na kufikiri kwa nini sasa hupendeki, uzidishapo madawa mengi, ukiachika utafanyaje?

Wengine wengi walifanya hivyo kutafuta mabwana wawapende, matokeo yalikuwa vifo na hivi sasa ni wakiwa."

Halafu ukaja wimbo uitwao 'Ushirikina' wa JKT Kimbunga Stereo. "Ingawa sumu ya ugonjwa ni dawa, lakini dawa zingine mbaya, ni za kupoteza uhai. Kuna msichana mmoja hapo zamani alimpenda mumewe, akaenda kwa mganga, kutafuta dawa ya mapenzi, akamlisha mumewe.

Bwana alipokula cha jioni hakutoka nje, asubuhi na mapema watu walikuta ameshakufa. Maisha ya mumewe sasa yameshapotea oo jama, alivyotengenea, wala haikuwa hivyo alifanya vibaya sana. Badala ya kupendwa sasa yamekuwa majuto anahangaika. Hilo ni fundisho kwa wanawake msifanye hivyo."

Hazikuwa nyimbo zenye mashairi mengi, ni machache tu lakini mazito, yanayoeleweka kwa urahisi na yenye mafunzo kwa jamii. Leo tunakuja na wimbo mwingine kabisa unaosapoti nyimbo hizi. Ni mwendelezo ule ule kuhusu ushirikina, lakini huu una kisa cha kushangaza.

Ulifyatuliwa na bendi ya Western mwaka 1973 ukapewa jina la 'Roza'. Kisa ni cha mwanamke mmoja ambaye alitaka kufanya kama baadhi ya wenzake 'kumtengeneza' mpenzi wake ili azidi kumpenda, kusahau wengine na kumuwezesha kupitiliza.

Akaenda kwa mganga wa kienyeji, lakini kilichomkuta huko ikawa ni historia. Alikwenda kwa mganga ambaye ni adui wa mpenzi wake. Na mganga alijua kabisa kuwa mteja huyu ni mpenzi wa adui yake. Halichogombania mimi na wewe hatukijui.

Mwanamke akataka dawa ya mapenzi maarufu kama 'limbwata.' Mganga badala ya kumpa dawa ya mapenzi, akampa sumu ya kwenda kummaliza mpenzi wake huyo mwanamke kwa sababu walikorofishana siku za nyuma.

Baada ya mwanaume kunywa ile dawa, iwe aliila kwenye chakula au maji ya kuoga, akaanza kuumwa badala ya kumpenda mpenzi wake huyo.

Huku na huku katika kutafuta 'kinachomtafuna' jamaa, ikagundulika kuwa alikula au kunywa sumu. Na alipewa kama dawa ya mapenzi na mpenzi wake.

Baada ya kugundua kila kitu ndipo alipomwita mpenzi wake na kuanza kumlaumu. Na lawana hizi zipo kwenye wimbo huo wa 'Western Jazz' unaoitwa 'Rosa'.

"Mapenzi yetu yamekuwa ni hasara Roza, mganga aliyekupa dawa ni adui yangu mama, penzi ulilotaka si penzi mwenzangu eee, dawa aliyekupa ni sumu mwenzangu eee, ndivyo ndivyo ulivyotaka toa roho yangu mama, kipi ulichokosa kutaka kuniua Roza, nilikuwa ninakupa mshahara wangu wote. Hiyo haikutosha mpaka wanitesa Roza, eee Roza, eee Roza, eee Roza, eee Roza mama."

Kwa kuangalia nyimbo zote tatu ni kwamba dawa za mapenzi zina hasara ya asilimia 90 kuliko faida. Nadhani kina mama na kina dada wanapaswa kuondokana na dhana hii. Hata kama kuna mmoja anataka kujaribu aache mara moja. Na wale ambao wameshajaribu waache.

Mbaraka ameshauri vizuri sana kabla ya kufanya yote, kwanza jiulize kwa nini hupendeki siku hizi tofauti na zamani. Ina maana kuna kitu kimepungua au kupunguzwa. Rejesha mapenzi ya kweli kwa mumeo kama zamani bila 'limbwata.' Hakuna mwanaume duniani anayechomoka kwa mwanamke anayemWonyesha mapenzi ya kweli.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

# Simu ya Sumu-7

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

DAN hakutaka kabisa kuamini kuwa Ziada hakufanya kitu kama hicho. Kichwani akawa anajiuliza kama siyo yeye huyo aliyefanya kitu hiki ni nani? ukimuondoa Ziada hakuna hawara yake hata mmoja anayemhisi.

Akili ikaendelea kumtuma kuwa aliyefanya hivyo ni yeye Ziada, ila kwa sasa anavunga hasa baaada ya kuona tayari ameshavuruga ndoa sasa ipo harijojo.

"Haya mama mimi naondoka, lakini naendelea kufanya uchunguzi wangu, kama wewe utakuwa unahusika, basi lazima nilipe kisasi. Na mimi nitavuruga huo uchumba wake na huyo mpenzi wako." Dan alinyanyuka baada ya kumaliza kuongea maneno hayo na kuanza kupiga hatua kutoka nje.

"Nakwambia hivi, rudi kambembeleze mkeo arudi nyumbani, wewe ni mwanaume. Mwenzangu miezi miwili tu umeanza kuchoka eee, na bado. Hayo ndiyo maisha ya ndoa, hayana raha peke yake, yana raha na karaha. Dan ngome ya fitina haivunjwi na watu fitina.

Hivi hukumwambia kuwa mtakapooana mtafanya sherehe, lakini maisha ya ndoa ni magumu uvumilivu unahitajika?" Dan alisindikizwa na maneno hayo kutoka kwa Ziada. Yalikuwa ni maneno ya hekima, lakini ndani yake ni kama mzungumzaji aliyazungumza kwa namna ya dhihaka na mzaha.

Aliondoka nyumbani kwa Ziada akiwa amechoka kimwili na kiakili. Tayari alikuwa ameshagombana na watu wawili ambao zamani alikuwa akiwapenda sana.

Ziada ambaye alikuwa mpenzi wake wake kwa zaidi ya miaka mitatu. Mkewe pia ambaye alianza naye kama mzaha, akienda kula kwa mama lishe ambaye ni mama mdogo wa Husna.

Anapomkuta alikuwa anajisikia raha, lakini siku ambayo hamkuti furaha inaondoka kiasi kwamba hata kuongea sana haongei. Tabia hiyo ilimfanya hata mama 'ake mdogo Husna kumshtukia.

"Huyu kaka kama Husna hayupo hana hata raha." Huwaambia wenzake anaokuja nao.

Wala haikuwa uongo, anapomkuta Dan kwake ni furaha moyoni wimbo mdomoni, "niwekee nyama nyingi kama kawaida yangu," hutania anapomkuta.

Yaliyoendelea ni historia hadi kufunga ndoa, lakini leo hii miezi miwili tu kila kitu kimeharibika. Kakosa mwana na maji ya moto.

Alianza kuyafikiria maneno aliyokuwa akijibiwa na Ziada. Kwa mara ya kwanza tangu afahamiane naye, leo



**"Hapana Tunda, yeye mwenyewe anatosha, kwa sababu alikuwa mpenzi wake kabla, wanaweza kukaa na kuelewana yakaisha. Ukienda tena na wewe kwenda kufanya ugomvi huko, yatazidi kuwa makubwa."**

ndiyo amejua kumbe Ziada anaongea vile. Ana maneno ya shombo ambayo hakuwahi kumsikia hata siku moja akigombana na mtu vile.

"Yule mwanamke kumbe naye anaongea namna ile?" Akawaza. Akakumbuka jinsi kaka yake Belo alivyomkataza Tunda kuongozana naye.

"Kaka twende wote tukamchambe maana atazoea siku nyingine, tutaenda kumsuta kwa rusha roho na mdundiko nyuma..."

"Hapana Tunda, yeye mwenyewe anatosha, kwa sababu alikuwa mpenzi wake kabla, wanaweza kukaa na kuelewana yakaisha. Ukienda tena na wewe kwenda kufanya ugomvi huko, yatazidi kuwa makubwa."

Dan alikumbuka mazungumzo ya kaka yake Belo na dada yake Tunda siku alipokwenda kwao.

"Mhh kweli kaka Belo alikuwa sahihi, kwa maneno yale ya Ziada kama ningekuwa na Tunda, pangechimbika na kweli yangezidi kuwa makubwa." Akazidi kuwaza.

***********************************

"Enheee kilichokuleta?"

"Mke wangu mimi nimekuja leo huku tuyazungumze tuyamalize..."

"Babu tafadhali ee mimi siyo mkeo ee."

"Mimi najua wewe bado mke wangu kwa sababu sijakupa talaka."

"Basi bora leo umekuja ili unipe talaka yangu."

"Mimi mbona sijui kosa langu, au wewe kuna kitu gani umefanya ili nikuache?" Dan akalalamika.

Alikuwa amekwenda ukweni, nyumbani kwa mama yake mdogo Tabia maeneo ya Mburahati ambapo si mbali sana na nyumbani kwake, Mabibo. Ndiko alikopeleka barua ya uchumba, mahari na sehemu harusi ilikofanyika. Alijua kabisa baada ya mtafaruku ule atakuwa amerejea kwao Mburahati.

"Kifupi nikwambie tu kuwa wewe huna mke hapa. Mkeo ni huyo uliyekuwa naye siku ile ukampa namba yangu, akanitukana weee, tani yake. Sasa nashangaa kilichokuleta nini? Umekuja tena ili mnitukane na hawara yako, au mmalize kabisa uhai wangu? Baba ee, fanya uondoke usinijazie nzi hapa."

Dan ambaye awali alidhani jambo lingekuwa dogo, lakini sasa ni kubwa na kile anapojaribu kugusa, linazidi kuwa gumu. Akaamua atumie njia nyingine ili lisuluhike. Nalo ni kukubali kosa na kuomba msamaha.

"Husna Mke wangu, unajua mimi ni binadamu, na binadamu upungufu ni jambo la kawaida, na tatizo lolote likitokea linalowahusu mke na mume, suluhisho lake ni kukaa na kulimaliza, sio kama hivi. Tatizo ni kulikabili na sio kulikimbia. Hata wazee wetu zamani waligombana lakini waliyamaliza wenyewe, halitakiwi kufika hata huku. Nakubali kuwa mimi nimekosa, nisamehe kwa hili."

Husna alimuangalia Dan kuanzia chini mpaka juu. Haikuwa angalia ya kawaida.

"Nadhani mwenzangu huyo ana kitu kingine cha ziada ndiyo maana ukamfuata." Akaongea kwa sauti ndogo, lakini ya msisitizo.

"Suluhisho la muafaka wa mimi na wewe ni kunipa talaka yangu tu."

"Husna hiyo haitowezekana, ujue mimi nakupenda sana, na ndiyo maana nimetoka nyumbani kuja huku. Kila nikipanda kitandani sipati usingizi, nimejitahidi kufanya kila njia lakini wapi, akili yangu haikai sawa kwa sababu yako. Kama kosa ni la kwanza tu, kwa nini ndoa yetu ivunjike kwa kosa moja. Kosa moja halivunji unyumba."

Husna alicheka kicheko cha kejeli, halafu akatikisa kichwa kuashiria kukataa.

"Hivi mfano wewe ndiye ungepigiwa siku na mwanamume wangu mimi akakuchamba kama alivyofanya huyo wako, ungenisamehe?"

Akauliza swali la ghafla na gumu. Dan akabaki kimya, hakujibu kitu, akabaki kumkodolea macho mkewe.

"Ni wazi ungeniacha." Akasaidiwa kujibu na muuliza swali.

"Basi inatosha mwanangu, ingia ndani, usipoteze nguvu zako bure kwa mwanamume kama huyu." Ilikuwa ni sauti ya Tabia, mama mdogo wa Husna ambaye muda mrefu alikuwa mlangoni akisikiliza kilichokuwa kikiendelea baina ya wanandoa hao.

"Mama hata wewe? Mi nilidhani ulipaswa kutusuluhisha, unazidi kuchochea moto!"

"Nini? Yaani umetoka huko uje kumbembeleza tena mwanangu akukubalie arudi tena jehanamu, ukamkutane na mahawara zako!"

"Mama, nyumbani kwangu unapaita jehanamu?"

"Ndiyo, tena zaidi ya jehanamu, angalia mwanangu alipokaa hapa na hivi sasa alivyo. Ulimkuta japo na shida zake, ananisaidia kuuza mama lishe, lakini alikuwa mzuri mrembo, leo hii yupo hivi.

Ulimchukua na afya yake nzuri, umekwenda kumfubaza mwanangu umepauka kama kitande cha muhogo. Hivi Husna mwanangu unajiona ulivyofubaa?" Akamgeukia binti yake.

"Miezi miwili tu tangu uolewe uko hivi ukikaa mwaka je, si utakuwa kama bibi kizee cha miaka 80!" Tabia alizidi kuponda. Akageuka na kumtazama tena mkwewe Dan. "Hapa mwanangu hatoki."

Dan alijiona ni mtu mwenye mkosi kuliko yeyote aliyewahi kugusa sayari hii ya dunia. Aliona dunia haimtaki. Amekuwa mtu wa kukosana na kila mtu. Kwanza amegombana na mkewe. Halafu akaenda kulaumiwa na ndugu zake. Akaenda kukutana na moto wa Ziada. Akarudi tena kwa mkewe Husna akakutana na moto mkubwa kushinda wa kwanza. Mama mkwe naye akaongeza petroli kwenye moto unaowaka.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# Harmonize, Esma wafanya kweli

UTATA unazidi kati ya mwanamuziki wa Bongo Fleva, Rajab Kahali, maarufu kama Harmonize na Esma, ambaye ni dada wa hasimu wake Diamond Platnumz, baada ya wawili hao kushirikiana kutoa singo.

Esma na Harmonize wamehusika katika wimbo 'Say Yes' ambao wamemshirikisha na DJ Seven.

Katika taarifa yake aliyochapisha kwenye ukurasa wake wa Instagram, Harmonize amesema Esma Platnumz ameweka sauti yake kwenye korasi ya wimbo huo.

Katika kile kinachoonekana wawili hao wana ukaribu zaidi, Konde Boy amemwagia sifa Esma kwa kusema sauti yake inapendeza.

"Eid Mubarak watu wangu wimbo wangu, Esma na Seven 'Say Yes' umetoka. Sasa sikutaka kusema hili lakini lazima nimtambue malkia. Hizo sauti za kike za chini zilizo pendezesha hapo kwenye baby kitendawili, macho Esma alifanya,"

Katika siku za hivi karibuni, msanii huyo wa zamani wa WCB na Esma wamekuwa na uhusiano mzuri.

# KAJALA AGOMA KUMTAJA MPENZI MPYA



MWIGIZAJI maarufu wa filamu Bongo, Frida Kajala Masanja, amesema hayuko tayari kumtambulisha mpenzi wake mpya.

Akizungumza na wanahabari baada ya kutua nchini Kenya, Kajala amesema hawezi kumtaja mtu ikiwa yuko nchini humo kwa ajili ya hafla ya hisani ya kuchangia watoto yatima itakayofanyika katika uwanja wa Nyayo, jijini Nairobi.

Kajala pia aliweka wazi kwamba mwanamuziki Mista Champagne ambaye alimuimbia wimbo ni rafiki yake na sio vinginevyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MOUNT AFUATILIWA

KLABU ya Arsenal inafuatilia hali ya Mason Mount kule Chelsea na wanaweza kushindana na Liverpool kumnunua kiungo huyo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 24 msimu huu wa joto. (***Goal***)

### ZUBIMENDI, NORMAND WAWINDWA

ARSENAL pia imetuma maskauti kumtathmini kiungo wa kati wa Hispania, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 24 na mlinzi wa Ufaransa, Robin le Normand mwenye umri wa miaka 26, ambao wote wanachezea Real Sociedad. (Daily Mail)

### OSIMHEN AANDALIWA DAU

KLABU ya Paris St-Germain inaandaa dau la pauni milioni 133 kwa mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen na itaingia kwenye nafasi nzuri mbele ya Chelsea, kwa ajili ya kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. (***Football Insider***)

### FIRMINO HUYO BARCA

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Roberto Firmino mwenye umri wa miaka 31 amekubali kujiunga na Barcelona mara mkataba wake na Liverpool utakapokamilika msimu huu wa joto. (***Daily Mail)***

### KOVACIC AWANIWA CITY

WASHAURI wa kiungo wa kati wa Chelsea na Croatia, Mateo Kovacic wamesafiri hadi London kuzungumza na Manchester City kuhusu uhamisho huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 akikaribia kuingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake. (***Sport Klub***)

### NDICKA ANYATIWA

LIVERPOOL na Tottenham Hotspur itajaribu kumsajili beki Mfaransa, Evan Ndicka mwenye umri wa miaka 23 kwa uhamisho wa bure mkataba wake na Eintracht Frankfurt utakapokamilika msimu huu wa joto. (***Football Insider***)

### 12 KUUZWA MAN

KLABU ya Manchester United itatarajia kuwauza wachezaji 12 wa kikosi cha kwanza msimu huu wa joto, akiwemo beki wa England, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 30, kipa wa Hispania, David de Gea mwenye miaka 32 na mshambuliaji wa Ufaransa, Anthony Martial, 27. (***Mirror***)

### MAMADASHVILI AWANIWA MAN

MANCHESTER United pia inamfikiria golikipa wa Valencia na Georgia mwenye thamani ya pauni milioni 45, Giorgi Mamadashvili mwenye umri wa miaka 22 kama mbadala wa David de Gea. (***Givemesport)***

### CARVALHO KURUHUSIWA

LIVERPOOL iko tayari kumruhusu mshambuliaji wa Ureno, Fabio Carvalho mwenye umri wa miaka 20 kuondoka kwa mkopo msimu ujao baada ya dakika 632 pekee za kucheza kikosi cha kwanza mwaka huu. (***Dakika 90)***

### NYOTA KIBAO WAWINDWA EPL

KLABU za Aston Villa, Newcastle, Liverpool na Tottenham Hotspur zote zilikuwa na maskauti kwenye robo fainali ya Ligi ya Europa kati ya Sporting Lisbon na Juventus siku ya Alhamisi pamoja na wageni wa kiungo wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 28, na winga wa Sporting, Marcus Edwards mwenye miaka 24, na kiungo wa kati wa Ureno, Pedro Goncalves mwenye miaka 24, ni miongoni mwa wachezaji wanaofanyiwa tathmini. (***90 min***)

### ALONSO HANA NIA

MLINZI wa Barcelona na Hispania, Marcos Alonso mwenye umri wa miaka 32 hana nia ya kuondoka katika klabu hiyo licha ya Inter Milan kumtaka. (***Mundo Deportivo***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# JESUS: TUTAPAMBANA MPAKA MWISHO EPL

## ●●● Ni baada ya Arsenal kutoka sare na Southampton yawaweka pabaya kwenye ubingwa na...

**LONDON,** England

GABRIEL Jesus ameapa Arsenal "itapigana hadi mwisho" kusaka ubingwa wa Ligi Kuu ya England baada ya kuwapa nafasi Manchester City kwa sare yao ya 3-3 dhidi ya Southampton, Ijumaa.

Arsenal walishindwa kushinda kwa mechi ya tatu mfululizo kwenye Ligi katika Uwanja wa Emirates, lakini walifanikiwa kuokoa pointi katika mchezo waliotoka nyuma kwa mabao 2-1 baada ya dakika 87.

Washikabunduki hao watasafiri kwenda kucheza na Man City Jumatano wakiwa na alama tano mbele ya wapinzani wao, ingawa wamecheza mechi mbili zaidi na kwa hiyo lazima washinde huko Manchester.

Badala ya kudondosha pointi mbili nyumbani, Jesus bado ana imani kabla ya safari hiyo kubwa ya kwenda Uwanja wa Etihad.

**"Hatutaki kuja hapa na kuzungumza kitu hasi kwa sababu tuna maoni mazuri. Tunachofanya msimu huu ni cha kushangaza. Ligi Kuu ya England ni ngumu," alisema akiiambia Sky Sports.**

"Sasa ni wakati mgumu. Ni wakati sasa wa kushikamana hadi mwisho. Bado tuna mambo mengi ya kufanya msimu huu. Haijaisha - bado tuna pointi tano mbele.

"Manchester City wana michezo miwili mkononi, lakini kama tunataka kuwa mabingwa lazima tuende huko ili kushinda mchezo huo - ni hayo tu.

"Sisi ndio timu changa zaidi kwenye ligi, ingawa sitoi visingizio. Wakati mwingine tunafanya vizuri na wakati mwingine tunafanya vibaya.

"Kila mtu anaweza kufanya makosa ndiyo maana ni muhimu sana kushikamana. Lolote linaweza kutokea.

"Ni wazi hatujafurahishwa na mechi tatu zilizopita. Tulipoteza pointi na tunajua hii ni kweli - hakuna mtu anayepaswa kutuambia. Tulipungua kidogo kiwango na umakini wetu.

"Hii ni Ligi Kuu. Ni ngumu sana kushinda mashindano haya. Lakini bado tupo, bado tunapambana na tutapambana hadi mwisho."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
BRIGHTON
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 2.24
X | 3.44
2 | 2.80

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP: NUNEZ MRADI WA MUDA MREFU LIVERPOOL



**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesema Darwin Nunez ni "mradi wa muda mrefu" hapo Liverpool amesisitiza kuwa mshambuliaji huyo "bado anazoea" maisha na Wekundu hao.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay, ambaye alihamia Anfield kutoka Benfica kabla ya msimu huu kwa ada ya awali ya pauni milioni 64, amefunga mabao 15 katika mechi 37 msimu wake wa kwanza akiwa na Liverpool, walio nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England na pointi tisa kutoka kwenye nafasi nne za juu. .

Ingawa, Nunez amepata wakati mgumu wa kucheza katika siku za hivi majuzi, akianza mechi moja tu kati ya nne za mwisho za Wekundu hao, huku Klopp akichagua wachezaji watatu mbele, Mohamed Salah, Cody Gakpo na Diogo Jota.

Lakini kocha huyo ambaye jana Jumamosi alimkosa Roberto Firmino kwenye mchezo dhidi ya Nottingham Forest kutokana na jeraha la misuli, amesisitiza kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 atapata nafasi nyingi kati ya sasa na mwisho wa msimu.

"Darwin ni mchezaji aliye na ustadi tofauti na wachezaji wetu wengine, ambayo ni nzuri," alisema Klopp wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari kabla ya mechi. "

"Atafunga mabao mengi, na tayari amefunga idadi nzuri. Lakini bila shaka, bado anabadilika. Kiingereza chake bado si kizuri, lakini tunalifanyia kazi hilo.

"Si muhimu kupitia msimu wa kwanza wakati ni ngumu kwa timu nzima. Mshambuliaji anawezaje kung'aa wakati timu nzima inatatizika? Haiwezekani, lakini amekuwa na wakati mzuri sana.

"Ninaelewa kwamba anataka kucheza kwa kutamani tangu mwanzo, lakini lazima tutafute njia ambayo inatufanyia kazi tena na kisha inafaa kwa wachezaji ambao tunaweza kuwatumia kwa nguvu maalum.

"Nina hali sawa kabisa na ninaelewa kuwa Darwin hayuko sawa kila wakati. Hatabasamu usoni mwangu anapogundua kuwa hataanza na kusema: 'asante, bosi'.

"Lakini unapokuwa na wachezaji watano au sita mbele, lazima ufanye maamuzi. Mlango uko wazi. Alikuja usiku mwingine na alikuwa wa kipekee. Ilikuwa njia sahihi kabisa. Kwa mechi tano ndani ya wiki mbili zijazo. , Darwin ataanza michezo, bila shaka."

# Tuchel hana tatizo na Muller

**MUNICH,** Ujerumani

THOMAS Tuchel amesisitiza kuwa hana tatizo lolote la kibinafsi kuhusu uamuzi wake wa kumuweka benchi Thomas Muller katika mechi zote mbili za robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya za Bayern Munich dhidi ya Manchester City.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 aliondolewa kwenye kikosi cha kwanza kule Manchester na Munich, huku Bayern ikiondolewa kwa jumla ya mabao 4-1 na hivyo kutolewa katika hatua ya nane bora kwa msimu wa tatu mfululizo.

Muller ndiye mchezaji mwenye mafanikio zaidi katika historia ya Bayern, akishinda mataji 11 ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, na mataji mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wa maisha yake ya kifahari akiwa na Bavaria hao.



Ana nafasi ya kunyakua taji lingine la ligi ya nyumbani msimu huu, lakini hilo ndilo kombe pekee ambalo Bayern wamebakia kuliwania baada ya kuondoka Ulaya na kufungwa na Freiburg katika robo ya kombe la Ujerumani, DFB-Pokal.

Ilidaiwa kwamba, Tuchel aliyeteuliwa hivi karibuni alitofautiana na gwiji wa klabu hiyo Muller, lakini kocha huyo amekanusha kama kuna tatizo lolote kati ya wawili hao.

"Mimi mwenyewe ni shabiki mkubwa wa Thomas Muller. Ana sifa ya kiwango cha juu duniani," alisema Tuchel katika mkutano na waandishi wa habari juzi.

"Mechi za Manchester hazijamfaa kikamilifu. Vinginevyo, pengine angecheza. Michezo mingi ni michezo ya Muller.

"Kila kitu kiko sawa kwa sasa. Nilifurahishwa na majibu yake kwenye uwanja wa mazoezi juzi. Nilifurahishwa sana. Aliishughulikia kwa njia ya kupigiwa mfano.

"Lakini lazima nifanye maamuzi yangu, wakati mwingine huwa magumu. Hakuna maelezo ya kibinafsi ndani yake. Kila mtu anapaswa kukubali katika hali ya ushindani." Tuchel amewataka Bayern waonyeshe ubabe zaidi katika michezo yao iliyosalia, akisema timu hiyo imekosa "azma na kasi".

"Ni muhimu jinsi timu inavyoshughulikia hali hiyo. Mengi yametokea msimu huu," alisema Tuchel. "Timu ina uzoefu mwingi."

Y | CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# Riadha U-18 kusimamiwa na serikali

Na Saada Akida

KATIBU Mtendaji Mkuu wa Baraza la Michezo Taifa (BMT), Neema Msitha amesema Serikali imedhamiria kuwekeza katika michezo na kuhakikisha wanasimama kwa ukamilifu na timu ya taifa ya riadha ya vijana chini ya miaka 18 na 20.

Timu hiyo iko katika maandalizi ya mashindano ya Afrika yanayotarajiwa kufanyika Aprili 27 hadi Mei 3, mwaka huu nchini Zambia.

Akizungumza na Nipashe jana, Msitha alisema tayari wanaendelea kuweka mambo mbalimbali kuwa sawa ili kukamilisha safari ya nchini humo.

Alieleza serikali inaendelea na mchakato wa kuhakikisha timu inapata mahitaji yote ikiwemo kambi nzuri na kuweza kusafiri na kurejea nchini na medali.

"Serikali ipo pamoja na tumefanya baadhi ya mambo na tunaendelea na safari ipo, vijana wanatakiwa kuzingatia nidhamu na Utamaduni wa kitanzania pindi watakapokuwa katika mashindano," alisema Msitha.

Aliwasihi wanariadha hao kwenda kuyafanyia kazi yale waliofundishwa na makocha wao pindi watakaokwenda katika mashindano.

"Mtambue serikali inatazama jicho lote kwenu, hivyo tunatarajia makubwa kutokana kwenu na sisi tunaendelea kufanyia kazi mambo mbalimbali.

"Muende kifua mbele na mkafanye vizuri na vyema mjitambue na kutafsiri kipaji chako na mmemwona kaka yenu Geay alikuwa jeshi la mtu mmoja na nyie mpo wengi," alisema Msitha.




Vijana wakifanya mazoezi ya mpira wa Kikapu katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

## *Simba yatanguliza mguu*

INATOKA UK 24

bao 1-0.

Salim amekaa kwenye mechi zote tatu bila kuruhusu wavu wake kuguswa na amecheza mechi hizo kutokana na kipa namba moja, Aishi Manula kuwa majeruhi.

Pamoja na ushindi huo, Simba ina kazi ya ziada ya kufanya itakapokwenda ugenini nchini Morocco kwenye mechi ya marudiano hatua ya robo fainali utakaochezwa Aprili 28 kwenye Uwanja wa Mohamed wa Tano, jijini Casablanca.

**WAJAZWA NOTI**

Baada ya ushindi huo, wachezaji wa Simba wamemwagiwa mamilioni ya fedha baada ya ahadi ya Rais wa heshima na muwekezaji wa klabu hiyo, Mohammed Dewji ambaye aliahidi kutoa Sh. Milioni 300. Ahadi hiyo imetolewa juzi usiku alipokutana na wachezaji hao kabla ya kucheza mechi ikiwa ni hamasa na sasa wanasubiri mzugo huo baada ya kufanikiwa kuibuka na ushindi.

Mo Dewji ni miongoni watu waliojitokeza uwanjani kwa ajili ya kusapoti Simba ikitafuta tiketi ya kucheza nusu fainali ya michuano hiyo kwa dakika 90 za mechi ya kwanza na 90 za pili kurejewa nchini Morocco. .

## Yanga: Ushindi ni lazima leo

INATOKA UK 24

bani, tumezungumza na wachezaji wetu na kuwapa mbinu mbalimbali kuelekea mchezo huo.

Tunatambua umuhimu wa ushindi wa mchezo huu, utakuwa mgumu kwa sababu tuko ugenini na tutaingia kwa nidhamu ya hali juu ili kufanikisha kuvuna pointi tatu muhimu za dakika 90 za kwanza," alisema Nabi.

Aliongeza wamewasoma wenyeji wao ni wazuri wakiwa nyumbani, wataingia uwanjani kwa tahadhari na kuhakikisha hawaruhusu bao lolote na kutumia vizuri nafasi wanazotengeneza.

Kocha wa Rivers United, Stanley Eguma alisema Yanga waliyokutana nayo msimu uliopita ni tofauti na ya sasa, hivyo anategemea mchezo kuwa mgumu ingawa malengo yao ni kuweza kuutumia vizuri uwanja wao wa nyumbani.

"Yanga imebadilika kwa maana ya aina ya uchezaji na hata wachezaji walionao kwa sasa ni tofauti, tunatarajia kupata mchezo mgumu kutoka kwao kwa sababu kitendo cha kuongoza kundi kinaonyesha wana timu zuri," alisema kocha huyo.

MECHI ZA USHINDI

"1" – NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" – NI TIMU KUTOKA SARE
"2" – NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 23/04/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3114 | Empoli vs Inter | 5.79 | 4.09 | 1.49 |
| 14:00 | 1188 | Reims vs Strasbourg | 1.90 | 3.50 | 3.60 |
| 14:00 | 5274 | West Bromwich vs Sunderland | 1.90 | 3.45 | 3.65 |
| 14:30 | 1377 | Heidenheim vs Holstein Kiel | 1.81 | 3.69 | 3.89 |
| 14:30 | 3800 | Sandhausen vs Paderborn | 3.68 | 3.63 | 1.88 |
| 14:30 | 5645 | Jahn Regensburg vs Kaiserslautern | 2.49 | 3.28 | 2.67 |
| 15:00 | 3199 | Elche vs Valencia | 3.99 | 3.39 | 1.84 |
| 15:00 | 3652 | Lugo vs Malaga | 3.36 | 3.01 | 2.18 |
| 15:30 | 1443 | PSV Eindhoven vs Ajax | 2.28 | 3.46 | 2.76 |
| 15:30 | 5403 | GO Ahead Eagles vs Fortuna Sittard | 1.92 | 3.45 | 3.60 |
| 16:00 | 1052 | Udinese vs Cremonese | 1.68 | 3.69 | 4.49 |
| 16:00 | 1468 | Lorient vs Toulouse | 2.25 | 3.55 | 2.75 |
| 16:00 | 1469 | AC Ajaccio vs Brest | 2.95 | 3.00 | 2.40 |
| 16:00 | 2397 | CF Estrela vs Belenenses | 1.62 | 3.71 | 4.81 |
| 16:00 | 3063 | Nantes vs Troyes | 1.61 | 3.81 | 4.81 |
| 16:00 | 3781 | Nice vs Clermont Foot | 1.75 | 3.45 | 4.39 |
| 16:00 | 4163 | Monza vs Fiorentina | 3.36 | 3.26 | 2.06 |
| 16:00 | 5046 | Newcastle vs Tottenham | 1.80 | 3.59 | 3.89 |
| 16:00 | 5086 | Bournemouth vs West Ham | 2.76 | 3.11 | 2.46 |
| 16:30 | 1638 | Wolfsburg W vs Arsenal W | 1.58 | 3.78 | 4.98 |
| 16:30 | 5506 | SC Freiburg vs Schalke 04 | 1.72 | 3.61 | 4.31 |
| 17:15 | 2920 | Pisa vs Bari | 2.31 | 2.94 | 3.15 |
| 17:15 | 4849 | Barcelona vs Atletico Madrid | 1.99 | 3.15 | 3.69 |
| 17:30 | 1571 | Portimonense vs Gil Vicente | 2.47 | 3.21 | 2.71 |
| 17:30 | 2944 | FC Zurich vs St. Gallen | 2.13 | 3.47 | 3.05 |
| 17:45 | 4396 | Feyenoord vs Utrecht | 1.33 | 5.03 | 7.24 |
| 18:00 | 3792 | Sturm Graz vs RB Salzburg | 2.92 | 3.28 | 2.16 |
| 18:05 | 1649 | Montpellier vs Rennes | 3.00 | 3.30 | 2.20 |
| 18:30 | 1929 | SuperSport Utd vs Amazulu | 2.00 | 3.13 | 3.71 |
| 18:30 | 2027 | Aberdeen vs Rangers | 5.21 | 4.31 | 1.51 |
| 18:30 | 5355 | Brighton vs Manchester Utd | 2.24 | 3.44 | 2.80 |
| 19:00 | 1087 | Galatasaray vs Fatih Karagumruk | 1.28 | 5.67 | 7.78 |
| 19:00 | 2218 | AC Milan vs Lecce | 1.47 | 3.95 | 6.40 |
| 19:30 | 1748 | OH Leuven vs Standard Liege | 2.50 | 3.48 | 2.52 |
| 19:30 | 2205 | Anderlecht vs Mechelen | 1.35 | 5.04 | 6.85 |
| 19:30 | 2216 | Brugge vs Eupen | 1.31 | 5.22 | 7.83 |
| 19:30 | 2284 | KAA Gent vs Oostende | 1.21 | 6.22 | 10.02 |
| 19:30 | 2685 | CSKA Moscow vs Lokomotiv Moscow | 1.87 | 3.46 | 3.77 |
| 19:30 | 3104 | Mirandes vs Burgos | 2.31 | 2.95 | 3.15 |
| 19:30 | 4427 | Mallorca vs Getafe | 2.26 | 2.75 | 3.51 |
| 20:00 | 2675 | Benfica vs GD Estoril | 1.10 | 7.84 | 19.09 |
| 20:00 | 5891 | Santa Clara vs GD Chaves | 2.57 | 3.12 | 2.67 |
| 20:30 | 5201 | Monchengladbach vs Union Berlin | 2.29 | 3.19 | 2.95 |
| 21:00 | 1634 | AZ Alkmaar vs Waalwick | 1.31 | 5.01 | 7.81 |
| 21:00 | 4553 | Olympiakos vs AEK Athens | 2.16 | 3.24 | 3.29 |
| 21:45 | 2684 | Lyon vs Marseille | 2.39 | 3.46 | 2.61 |
| 21:45 | 5853 | Juventus vs Napoli | 2.69 | 2.94 | 2.64 |
| 22:00 | 1682 | Alaves vs Leganes | 1.71 | 3.34 | 4.89 |
| 22:00 | 3192 | Sevilla FC vs Villarreal | 2.75 | 3.20 | 2.41 |
| 22:30 | 1475 | FC Arouca vs FC Vizela | 2.56 | 3.07 | 2.71 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Nipashe
Jumapili Aprili 23, 2023



Jesus: Tutapambana mpaka mwisho UK. 21



Mshambuliaji wa Simba, Jean Baleke akiifungia Simba bao kwenye mchezo wa Ligi ya mabingwa Afrika dhidi ya Waydad Casablanca katika uwanja wa Benjamin Mkapa jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA YATANGULIZA MGUU NUSU FAINALI

●●● Yaweka tena rekodi ya kumfunga bingwa mtetezi, wachezaji wajazwa noti Mil 300..

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KWA mara nyingine tena jana jioni timu ya Simba imeweka rekodi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa kumfunga bingwa mtetezi wa kombe la Ligi ya mabingwa Afrika, ilipopata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Wydad Casablanca Athletic kutoka nchini Morocco.

Bao pekee lililoendeleza rekodi hiyo lilifungwa na Jean Baleke dakika ya 30, alipounganisha shuti la Kibu Denis, ikiwa ni mechi ya mkondo wa kwanza wa pambano la robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alikuwa ni Baleke mwenyewe aliyefanyiwa madhambi mbali kidogo na lango, lakini shuti la mpira wa faulo ulipigwa na Saidi Ntibazonkiza uliwababatiza mabeki wa Wydad Casablanca na kuzua kizaazaa langoni, kabla Kibu kuachia shuti kali ambalo lilionekana kama linatinga wavuni, lakini Baleke aliunganisha mpira huo na mguu wa kulia kuhakikisha mpira huo unaingia kwa usahihi zaidi.

Hii si mara ya kwanza kwa Simba kupata ushindi dhidi ya Mabingwa Watetezi wa Afrika, kwani imeshafanya hivyo mwaka 2003 ilipoichapa Zamalek ya Misri bao 1-0 nchini lililofungwa na Emmanuel Gabriel, na ikaenda ugenini na kufungwa bao 1-0, lakini ikaivua ubingwa na kutinga hatua ya makundi kwa mikwaju ya penalti 4-3.

Mwaka 2019, iliichapa Al Ahly bao 1-0 nyumbani likifungwa na Meddie Kagere na 2021, iliichapa tena Al Ahly bao 1-0 likiwekwa ndani ya wavu na Luis Miquissone.

Mechi ya jana ilianza taratibu kila timu ikijaribu kusoma mchezo wa mwenzake, lakini kwenye dakika ya nne nusura Wydad Casablanca ipate bao kutokana na uzembe wa walinzi wa Simba.

Henock Inonga alimrudishia mpira Joash Onyango ambaye hakuwepo na mpira huo ukanaswa na Ayman El Hassouni, lakini purukushani zake za kutaka kuukwamisha mpira wavuni zikaishia mpira huo kutoka nje.

Dakika mbili baadaye Ntibazonkiza angeweza kuwa wa kwanza kupata bao baada ya shuti lake kali kutoka kidogo nje ya lango, akiwa amemegewa pande kutoka kwa Clatous Chama.

Beki wa Wydad raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Arsene Zola, nusura afunge bao dakika ya 15 alipounganisha mpira kwa kichwa kutokana na kona iliyochongwa na Yahia Attiyah Allah, lakini ukatoka nje kidogo ya lango.

Baada ya Simba kupata bao, ingeweza kupata lingine dakika ya 32, kwani pasi murua ya Chama ilikwenda kwenye miguu ya Sadio Kanoute ambaye aliachia kombora lililompita kipa Youssef El Motie na ulionekana kama ungejaa wavuni, lakini ukatoka sentimeta chache.

Kipindi cha pili, Mabingwa hao watetezi walifanya mabadiliko ya pamoja ya wachezaji kadhaa ambayo yaliwapa nguvu ya kufanya mashambulizi, lakini mabeki wa Simba wakiongozwa na Inonga walikaa imara huku golikipa, Ally Salim akiibuka tena kuwa shujaa kwa kuokoa mipira kadhaa ya hatari.

Hii inakuwa ni mechi yake ya tatu kucheza kwa dakika 90 na ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Alicheza mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania bara dhidi ya Ihefu kwenye Uwanja wa Highland Estates Simba ikashinda mabao 2-0, ikasimama tena langoni kwenye mechi dhidi ya watani wa jadi Yanga, timu yake ikaondoka na ushindi wa mabao 2-0, kabla ya jana tena ikishinda

INAENDELEA UK 23

## Yanga: Ushindi ni lazima leo

**Na Saada Akida**

VYOVYOTE itakavyokuwa, iwe jua, iwe mvua lazima tuondoke na ushindi leo. Hayo ni maneno ya Yanga kuelekea mchezo wao wa kwanza leo wa robo fainali ya kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Rivers United.

Yanga wanashuka dimbani kusaka ushindi muhimu ili kulipa kisasi pamoja na kumaliza dakika 90 ya kipindi cha kwanza ugenini kwa kumfunga mwenyeji wao Rivers United katika uwanja wa Kimataifa wa Godswill Akpabio mjini Uyo nchini Nigeria.

Rivers mara zote wamekuwa wagumu katika uwanja wao nyumbani hasa walipomfunga Wydad Casablanca mabao 2-0 katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika na kutolewa kwa kufungwa mabao 6 walipokwenda kucheza nchini Morocco kwenye mchezo wa marudiano.

Yanga wanahitaji kuvunja mfupa ambao ulimshinda Wydad nchini Nigeria pamoja na kuhitaji kulipa kisasi kwa Rivers United ambao msimu uliopita walishinda mechi zote mbili nyumbani na ugenini kwenye hatua ya awali ya Ligi ya mabingwa Afrika.

Yanga inahitaji kupata matokeo mazuri ili wasiwe na kibarua kigumu katika mechi ya kurudiana jinni Dar es Salaam, Tanzania mchezo utakaopigwa Aprili 30 mwaka huu uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddin Nabi alisema wamefanya maandalizi mazuri na wamechukua tahadhari kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo huo.

Alisema maandalizi ya mwisho yamekamilika na wachezaji wako tayari kuwakabili Rivers United ili kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huo ambao ni muhimu kwao ili wasiwe na mzigo mzito katika mchezo wa marudiano.

"Tuna asilimia 80 ya kufuzu nusu fainali, tumejiandaa vizuri kuhakikisha tunashinda mechi ya kesho (leo). Tunawafahamu Rivers United kwani tumewahi kucheza nao wanakuwa bora zaidi wanapokuwa katika uwanja wao nyum-

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >